





**Mitindo** jezi mpya Simba gumzo

UKURASA 20



**Drake**, Soulja Boy hofu tupu wakizindua albam zao mpya

UKURASA 20


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 5, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya

ISSN 0856 • No. 0580694

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




RIPOTI MAALUM

# Uhaba maeneo maziko mtihani mgumu Dar

• **Yaliyotumika** tangu ukoloni yaendelea, manispaa zakiri, zinapigania majibu... *Endelea ukurasa 4*



Sehemu ya makaburi ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. Licha ya eneo hilo kujaa lakini shughuli za maziko zimekuwa zikifanyika. **PICHA: MIRAJI MSALA**


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**SERIKALI YATAMBA KUDHIBITI WIZI WA MTANDAO KWA 90%**


## Daktari amfumua nyuzi mgonjwa kisa pesa

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play
App Store




## Maeneo matano kuchunguzwa kupanda kwa bei za mafuta

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA QUEENS-TUNATAKA UBINGWA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Maeneo 5 kuchunguzwa kupaa bei mafuta

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI iliyoundwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuchunguza upandaji bei ya mafuta nchini, imeanza kazi na maeneo matano yatafanyiwa uchunguzi ikiwamo mfumo wa uagizaji kwa pamoja.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema hayo jana jijini hapa akiongeza kuwa kamati hiyo pia imepewa siku 14 kukamilisha kazi hiyo na kutoa taarifa serikalini juu ya mambo itakayobaini.

"Kama mnavyofahamu EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji), walipandisha bei ya mafuta Septemba Mosi, mwaka huu na baadaye bei zile zikasitishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na kuagiza ziendelee kutumika bei za Agosti ili kutoa muda kwa kamati aliyoiunda kuangalia upya bei za mafuta," alisema Msigwa

Msigwa alisema kamati hiyo tayari imeshakutana na imeanza kazi na kwamba katika mambo itakayobaini, itatoa maoni yake kwa kuwa lengo la serikali ni kuona bei za mafuta zinakuwa nafuu kwa wananchi.

"Na pia kama bei zitatakiwa zipande basi zinatakiwa kuwapo sababu za msingi," alisisitiza Msigwa. Mambo mengine ya uchunguzi, kwa mujibu wa Msigwa, ni pamoja na kuangalia mfumo mzima wa ukokotoaji wa bei, utaratibu wa serikali wa ununuzi wa mfuta kwa pamoja na kuangalia tozo mbalimbali zilizomo kwenye mafuta.

"Pia Kamati hii imeelekezwa kuangalia kampuni ambazo zinaagiza mafuta hayo kutoka nje ya nchi kuja hapa nchini. Kamati hiyo inakwenda kuangalia utaratibu uliowekwa kwenye bandari za Dar es Salaam na Mtwara ambako ndiko mafuta yanashushwa.

"Lengo la serikali hasa ni kujua sababu za kupanda kwa mafuta lakini pia kuangalia maeneo ambayo yanaweza kushughulikiwa ili Watanzania waendelee kupata mafuta kwa bei nafuu," alisema.

Msigwa alisema serikali inalifanyia kazi jambo hilo kwa ukaribu na inatambua kupanda kwa mafuta kuna madhara kwenye maisha ya watu na uchumi.

"Kamati ilianza kazi Septemba 2 na itafanya kazi kwa muda wa wiki mbili ambapo Septemba 16, mwaka huu itatoa taarifa juu ya nini imebaini katika mchakato huo wa kufuatilia bei ya mafuta" alisema.

Katika hatua nyingine, Msigwa aliwakumbusha Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari na kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Pia alisema serikali inasisitiza kuwa chanjo ya corona ni ya hiari na wataalamu wanasisitiza kuwa ni salama na hadi sasa zaidi ya Watanzania 325,000 wamechanja.

"Serikali inawasihi wananchi ambao wako katika makundi hatarishi kujitokeza kupokea chanjo hizo. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea kufanya juhudi za kupata chanjo zaidi kwa ajili ya Watanzania. Yako matumaini makubwa ya kupata chanjo baada ya shehena ya dozi 1,058,400 iliyoletwa Julai 24 kutoka Marekani kuisha," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa, akishirikiana na wananchi kusafisha eneo la ujenzi wa Kituo cha Afya cha Narung'ombe, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, jana. **PICHA: OWM**

# Daktari amfumua mgonjwa nyuzi kisa kukosa pesa

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, Tabibu wa Zahanati wa Kerenge, kata ya Kibaoni, wilayani Korogwe, Jackson Meli, anadaiwa kumfumua nyuzi majeruhi wa ajali ya pikipiki aliyeshindwa kulipa Sh. 10,000 za matibabu.

Tukio hilo ambalo video yake ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii, lilizua taharuki kijijini humo, huku tabibu huyo akithibitisha kulifanya akihojiwa na Diwani wa Kata Kerenge, Abdallah Robo, kwa madai kuwa alitaka kulipwa gharama za matibabu.

Waliokumbwa na mkasa huo ambao ulitokea Julai 28, mwaka huu ni Zubeda Ngereza na kijana wa pikipiki ambao walipata ajali wakiwa njiani na chombo hicho cha usafiri na kupelekwa katika zahanati hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Halfani Magani, alikiri kuwapo kwa tukio hilo na kwamba tabibu huyo ambaye alishaondolewa katika zahanati hiyo, aliwapokea majeruhi hao na kuwapa huduma.

Alisema huduma ambazo aliwapatia zilikuwa pamoja na kumshona mama huyo nyuzi katika eneo la mkono na kumfunga bandeji na dereva wa bodaboda alifungwa bandeji maeneo alikoumia.

Kwa mujibu wa Magani, baada ya huduma hiyo ndipo tabibu alipodai gharama za matibabu ambazo kwa huyo mama zilikuwa ni Sh. 10,000 na aliposhindwa kulipa kwa wakati huo, akafanya uamuzi wa kumfumua nyuzi.

"Halmashauri tulipokea taarifa hizi na kwa kushirikiana na polisi tulifika eneo la tukio na kumkamata tabibu huyo ambaye alikaa chini ya uangalizi katika Kituo cha Polisi Korogwe, kuanzia Julai 28 hadi 30 kisha alisimamishwa kazi na kumpatia hati ya mashtaka kwa kuzingatia kanuni za utumishi wa umma,"alisema.

Alisema halmashauri imeliandikia Baraza la Matatibu Tanzania kwa ajili ya kuchukua hatua zaidi kwa kuwa ni kinyume na kanuni za utabibu. Kuhusu kupeleka tabibu mwingine, Magani alisema katika zahanati hiyo alikuwapo tabibu huyo na manesi wawili na sasa wamebaki hao manesi na kwamba upo uhaba wa watumishi wa afya na zipo zahanati ambazo kuna mtumishi mmoja.

**VIONGOZI WANENA**

Diwani Robo akisimulia kwa upande wake, alisema wakati wakiwa kwenye kikao na Mkuu wa Wilaya alipigiwa simu na mwananchi kumjulisha kuhusiana na tukio hilo.

"Nilijulishwa kuwa kuna mama amefikishwa kwenye Zahanati ya Kerenge baada ya kupata ajali ya pikipiki wakati akimpeleka mtoto wake kituo cha afya. Wakiwa njiani walipata ajali na mama huyo alichanika kwenye kiwiko cha mkono ndipo wakaenda katika zahanati hii ya kijiji," alisema.

Alisema huduma walizopewa ni pamoja na mama huyo kushonwa eneo la jeraha na kufungwa bandeji na dereva wa bodaboda alifungwa bandeji.

"Baada ya huduma ndipo tabibu akamwambia: 'mama nimeshamaliza kazi naomba ulipe hela' yule mama akamwambia 'kwa sasa sina hela, naomba ukae na hii pikipiki, twende nyumbani kuchukua tukuletee.' Yule tabibu akamwambia, 'ili ukalete fedha ngoja nikuondoe hizi nyuzi nilizokushona' akamfumua na bandegi akawany'ofoa wote," alisimulia.

**Imeandaliwa na Salome Kitomari na Romana Mallya**

## Wakazi Magomeni kukaa miaka mitano bure

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamuriho, amesema wakazi 644 wa Magomeni Kota watakaa miaka mitano bila kulipa kodi ya pango kama walivyoahidiwa na serikali.

Chamuriho aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na wakazi wa makazi mapya Magomeni Kota ambao wanatarajiwa kuhamia mwezi ujao.

Alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 99 na kwamba kilichobakia ni kufunga umeme, kuandaa miongozo na mkataba wa wapangaji na kuweka lifti kutokana na majengo mengine kuwa gorofa tisa.

Alisema serikali si kigeugeu na kwamba ahadi iliyotolewa na Rais Hayati John Magufuli kwa wakazi hao itatekelezwa kwa kuhakikisha watakaohamia wamehakikiwa na Ofisi ya Rais, uongozi wa mtaa na kamati ya Magomeni Kota inayosimamia mchakato huo.

"Ambao tuliwatoa hapo ni hao hao watarudi katika majengo hayo. Malengo hayajabadilika hadi sasa na wale wanaosema orodha ya majina hatujui wamepata wapi. Mtaingia katika nyumba kama mlivyoahidiwa msiwe na wasiwasi.

"Kwa sababu tunamalizia orodha ya uhakiki wa majina wale ambao walikuwa pale watarudi katika kaya 644 watakuwa wanufaika. Mradi una nyumba 656 ambazo ni nyumba 12 zaidi ya kaya 644 zilizokuwapo. Ongezeko hilo ni kwa ajili ya wasimamizi wa majengo haya," alifafanua Chamuriho. Aidha, alibainisha kuwa utaratibu unaoendelea kwa sasa ni kuandaa mwongozo ikiwamo ya wakazi hao watakavyochangia fedha kwenye huduma za maji, umeme, uondoshaji taka na mfumo wa majitaka na ulinzi kwa ajili ya kutunza makazi hayo.

Chamuriho alisema mradi huo ulianza mwaka 2016 kwa kujenga majengo matano ya ghorofa yenye kaya 644, zikiwamo 12 za wasimamizi na eneo la kufanyia biashara mdogo kama soko, umekwishatumia Sh. bilioni 52.1.

Mwenyekiti wa Wakazi wa Magomeni Kota, George Abel, alishukuru serikali kwa kutoa kauli ya matumaini kwa wakazi hao na kwamba matarajio ni kuhamia mwezi ujao kama waliyoahidiwa na serikali huku akiwataka kujiandaa kuchangia gharama za ankra mbalimbali.

# HABARI KITAIFA

## Polisi wadaiwa kuvuruga kongamano CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimedai Jeshi la Polisi limefunga ofisi zake za wilaya ya Musoma Mjini na kubeba mahema na viti vilivyoandaliwa kwa ajili ya kongamano.

Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema jana kulikuwa na kongamano la katiba mpya lililokuwa limeandaliwa na Baraza la Vijana Chadema (BAVICHA) wilayani humo.

Alisema Alhamisi Mkuu wa Mkoa wa Mara alitangaza siku ya jana ni kwa ajili ya usafi mkoani humo na kwamba mwananchi ambaye hatashiriki atalipa faini ya Sh. 50,000.

"BAVICHA waliwatangazia wanachama wake na wananchi waje na vifaa vya usafi ili washiriki kufanya usafi na mkuu wa mkoa baadaye wataendelea na kongamano lililokuwa lifanyike katika ofisi za chama wilaya," alisema.

Mrema alidai usiku wa kuamkia jana majira ya saa 7:30 usiku, polisi walivamia ofisi hizo na kuchukua mahema na viti vilivyokuwa tayari kushiriki kongamano hilo.

"Leo (jana) asubuhi polisi wamezingira na kufunga kwa kofuli lao geti la kuingilia ofisini na hakuna dalili kuwa wanafanya usafi na badala yake wamewakamata wananchi ambao walikuwa tayari kushiriki ufanyaji usafi," alidai.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni watu sita ambao ni Patrick Nyabagwe, George Rubare Nahima Seleman, Magret Emanuel, Musila Juma na Medard Shija.

Mrema alisema CHADEMA inafuatilia tukio hilo na kulaani kitu walichokiita ni ukiukwaji na ukandamizaji wa haki dhidi ya raia unaoendelea kufanywa na Jeshi la Polisi.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Longinus Tibishubwamu, alikanusha madai hayo ya CHADEMA kuwa polisi imechukua vitu vyao.

"Leo (jana) tulikuwa na programu ya usafi iliyohusisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama, mashirika ya umma, asasi zisizo za kiserikali, wananchi, polisi tulipangiwa eneo la Nyakato ambako ofisi za CHADEMA zipo na eneo lingine ambalo tunaendelea na usafi sasa hivi.

"Kwenye mtandao tuliona mambo mengi wanaandika kuhusu kufanya kongamano la katiba mpya, inaonekana ni kama wanataka kuleta vurugu, nilitoa tamko kama kitu hiki kipo kwenye mkoa huu hatutakubali kifanyike tutakizuia kwa nguvu zote, lakini kwamba tumekwenda kuchukua vitu ofisini kwao si kweli."

Kuhusu kukamata watu, Kamanda huyo alisema tangu juzi (Alhamis) walikuwa na operesheni ya kukamata vitu vya wizi na kueleza yawezekana na hivyo vimechukuliwa katika mtiririko huo.

"Labda mahema yamechukuliwa kwa kutuhumiwa kuwa ni vitu vya wizi, tumefanya operesheni sehemu nyingi," alisema.

Alipoulizwa kama ni kweli polisi walifika katika ofisi hizo na kuchukua vitu hivyo, Kamanda huyo alisema hata jambo likifanywa na ulinzi shirikishi au watendaji wa kata wanasema ni polisi.

Kuhusu madai kuwa kuna wananchi wamekamatwa alisema operesheni yao waliyoifanya imekamata watu sita kwa tuhuma za vitu vya wizi.

"Kwenye makosa ya wizi tunakamata mtu yeyote tunachunguza akionekana msafi tunamwachia lakini sasa mtu akikamatwa anajivalisha shati kuwa 'mimi nimekamatwa kisiasa' hatuko kisiasa muda wote," alisema.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Thobias Mwanakatwe**



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akiwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Afya Bugisi cha Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Dk. Kathleen Costigan, wakimjulia hali mtoto mwenye utapiamlo ambaye anatibiwa katika kituo hicho, jana. Mkuu huyo, amewataka wazazi kuwapeleka watoto hospitalini wanapowaona wana matatizo ya kiafya badala ya kukimbilia kwa waganga wa kienyeji. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Serikali yatamba kudhibiti wizi mtandaoni asilimia 90

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema serikali imethibiti matukio ya wizi wa mtandaoni kwa zaidi ya asilimia 90.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam baada ya kutembelea Shirika la Posta Tanzania ambalo kesho Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajia kuzindua Kituo cha Huduma za Pamoja (One Stop Centre) kilichoanzishwa na shirika hilo.

Ndugulile alisema mafanikio ya kuyapunguza matukio hayo yametokana na serikali kuanzisha kituo ambacho kinapokea malalamiko na kuyashughulikia.

Alisema mpaka sasa kituo hicho kimepokea malalamiko 31,000 na kuwataka wananchi wanaoendelea kupata ujumbe na kupigiwa simu za utapeli, wapeleke malalamiko yao kwenye kituo hicho.

Kuhusu Shirika la Posta, Dk. Ndugulile alisema kuanzishwa kwa kituo hicho kutawezesha huduma mbalimbali za kiserikali kupatikana humo na kuwapunguzia mzunguko wananchi kwenda ofisi moja na nyingine.

"Shirika la Posta imeibuka kidedea baada ya kushindanishwa na mashirika ya Posta mbalimbali Afrika na limeaminiwa katika utoaji wake wa huduma," alisema.

Waziri Ndugulile alisema mikakati iliyopo ni kuendelea kutoa huduma na kuongeza taasisi zingine katika mfumo huo wa pamoja ambao unaenda kuondoa mfumo wa kizamani na kuingia kidigitali.

"Huduma hii inaanza kwa awamu, tumeanza mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma na kisha baadaye itasambaa kwenye mikoa mingine kwa awamu tofauti," alisema.

Alisema wanaendelea kuongeza wigo wa utoaji huduma katika shirika hilo kwa kidigitali ndani na nje ya nchi.

Kaimu Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo, alisema tangu kuzinduliwa kwa huduma ya duka mtandao, shirika limeingiza faida ya Sh. milioni 300.

Alisema mfanyabiashara anapojiunga katika huduma hiyo ya mtandao na kuuza bidhaa zake shirika linapata asilimia tatu ya bei ya bidhaa sambamba na gharama za usafirishaji.

Mbodo alisema shirika linaendelea kuboresha huduma zake na kwa mwaka wa 2020/21 limeingiza faida ya Sh. bilioni tatu.

"Mabadiliko ya mfumo wa kidigitali yataenda kwa awamu tatu hadi kufikia mwezi Desemba, mwakani, mikoa isiyopungua 10 itakuwa imepata huduma ya pamoja kwa ofisi zote za kiserikali kuwa katika ofisi moja,"alisema.

Alisema baada ya mikoa hiyo miwili Dar es Salaam na Dodoma, watakwenda Mwanza, Kigoma, Arusha, Mbeya, Zanzibar, Mji Magharibi, Chakechake Pemba, Lindi, Tanga na Morogoro.

Alisema wanatarajia awamu ya pili kuanza mwaka wa fedha 2023/24 kwa kuhusisha mikoa ya Pwani, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Kilimanjaro, Tabora, Mara, Kagera, Shinyanga, Lindi, Simiyu, Mtwara, Manyara, Songwe, Katavi, Njombe na Geita.

Alisema ifikapo Desemba, 2025 shirika litajizatiti kufikisha Huduma ya Pamoja kwa ngazi ya wilaya ili kuwafikia wananchi zaidi.

## Waombaji 31,400 wathibitisha vyuo vya kujiunga

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imesema waombaji 31,395 kati ya 35,548 waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja, wameshajithibitisha chuo kimojawapo.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa udahili wa shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Prof. Kihampa alisema awamu ya pili ya udahili imekamilika na kuthibitisha udahili kwa waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja awamu ya kwanza itafungwa kesho.

"Mchakato utakaoendelea ni vyuo kuchakata na kuidhinisha maombi yua udahili yaliyopokewa, kukamilisha majina ya waliodahiliwa katika awamu ya pili na kutangazwa na vyuo husika Septemba 18, mwaka huu," alisema.

Awamu ya tatu ya udahili, alisema itafanyika kwa siku saba kuanzia Septemba 18, hivyo kuwataka waombaji ambao bado hawajatuma maombi yao wayatume kwa usahihi kwenye vyuo walivyovipenda.

Prof. Kihampa aliwataka waombaji wakati wanaomba, wasome miongozo ya sifa ya kujiunga na programu husika ili kuona kama wanakidhi vigezo kabla ya kutuma maombi.

"Waombaji wenye changamoto ya kupokea namba za siri ya kujithibitisha katika chuo kimojawapo, wanaelekezwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa namba maalum ya siri," alisema.

Pia tume hiyo imezitaka taasisi za elimu ya juu zinazofanya udahili huo zihakikishe zinaruhusu waombaji kuingia katika mifumo yao na kuwapa neno la siri (password) na jina (username).

"Taasisi zihakikishe waombaji wote wanajithibitisha wao wenyewe kupitia akaunti zao na si vinginevyo, waombaji wanaotaka kubadili uthibitisho wao, waingie katika akaunti za vyuo walivyothibitisha na kufuta uthibitisho wao wa awali ili wajithibitishe katika chuo kingine wanachopenda," alisema.

Prof. Kihampa alisema tume inawatoa hofu waombaji wa udahili wanaoshiriki mafunzo kwa mujibu wa sheria katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwa muda wa kujithibitisha utaongezwa ili wapate nafasi hiyo kabla ya mwaka wa masomo kuanza.

RIPOTI MAALUM

# Uhaba wa maeneo ya kuzikia mtihani mgumu Dar es Salaam

**Na Waandishi Wetu**

UNAPOTAJA Dar es Salaam, unagusa lililokuwa jiji kuu kihistoria na la kibiashara na hadi leo hii limefurika wakazi wanaokadiriwa kumiliki asilimia 10 ya Watanzania wote.

Hao ni zao la mafuriko ya wahamiaji 'wanaozamia' kusaka riziki kuanzia ajira rasmi na zisizo rasmi, bila kusahau huduma muhimu ngazi ya kitaifa, ilhali hata wategemezi wanaowawezesha baada ya maisha 'kuwakubali' wako huko.

Hapo hukosi kuitaja hospitali kuu nchini, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ikiwa na huduma za mwisho nchini kwa yaliyoshindikana huko kuanzia zahanati hadi hospitali za rufani za kanda.

Muhimbili yenye mafuriko ya wagonjwa wa hali na kada tofauti, sasa ina wabia palepale ilipo wenye majukumu kama yake: Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI); Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI); na waelimishaji Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili (MUHAS).

Nje ya geti nako kuna hospitali binafsi lukuki zenye huduma kiwango cha juu, nazo zikivuta wagonjwa wengi kuletwa Dar es Salaam kwa mtindo uleule wa rufani kwenda Muhimbili.

Hiyo inajenga maana gani? Mbali na idadi kubwa ya wakazi, hata kwa hesabu ya macho Dar es Salaam ina nyongeza ya idadi kubwa ya vifo hospitalini.

Je, mahali pa kuzika panawiana na hitaji hilo? Jibu la uzoefu wa ukazi, pia ushuhuda unaangukia 'hapana'.

Dar es Salaam inapanuka kwa kasi. Maeneo kama Tegeta, Gezaulole, Buza na Bunju ambako kulikuwa shamba hadi mwanzoni mwa miaka 1980, leo hii ni miji kamili iliyojengeka.

Pia makaburi mapya wakati huo kama ya Temeke Wailes yalioanzishwa miaka ya karibuni kuchukua nafasi ya Chang'ombe, yalishajaa siku nyingi.

Hata hivyo, makaburi hayo Chang'ombe yanayozidi umri wa uhuru wa nchi, kama ilivyo kwa wabia wake wa umri Kisutu na Kinondoni, ukifika kwa kuona pamejaa lakini mshangao maziko yanaendelea kila siku.

Maeneo mengine mapya ya kuzikia yaliyoanzishwa kwenye miji mipya kama Kinyerezi ambako watu wanakukimbilia, nako kumeshajaa.

Hiyo ndio hali halisi katika wilaya tano za Mkoa wa Dar es Salaam ambako hata ukaguzi wa kawaida kila siku ni kawaida kuona kwenye maeneo ya kuzikia kuna ama watu wanazika au kuandaa maziko, ikitoa jibu la vifo vingi na kuacha swali wanazikaje katika makaburi kongwe?

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 ilibaini Dar es Salaam ambayo ni kitovu cha shughuli za kibiashara na utawala kwa kiasi fulani, ilikuwa na wakazi milioni 4.4.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) ya Septemba 2017, inabainisha Tanzania ina wastani wa vifo saba katika kila watu 1,000 kwa mwaka.

Ni takwimu zinazotoa tafsiri kuwapo vifo vya watu 30,800 Dar es Salaam, sawa na vifo 84 kila siku kwa kuzingatia idadi ya wakazi milioni 4.4 waliokuwamo mkoani humo mwaka 2012.

**MIKAKATI MANISPAA**

Ofisa Uhusiano wa Manispaa ya Kinondoni, Sebastian Mhowera, akizungumza na Nipashe Jumapili kuhusu suala hilo, anasema mbadala wa makaburi ya Kinondoni ni kuanzishwa kwa eneo jipya la Kondo lililoko Tegeta wilayani humo.

Anasema makaburi mengine yaliyomo ndani ya manispaa hiyo yanajumuisha yanayomilikiwa kimila, kidini na watu binafsi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Sinza A, Ally Mgaya, akizungumzia hali ya makaburi ya Sinza wilayani Kinondoni, anasema bado wanaendelea kuzika kwenye eneo hilo.

"Bado hayajajaa, wanaothibitisha kujaa ni halmashauri, wakifanya hivyo maana yake tunasitisha, bado watu wanaendelea kuzika," anasema.

Katika kufuatilia uhalisia uliopo kwenye Makaburi ya Sinza, Nipashe Jumapili ilizuru kwenye eneo hilo na kushuhudia wachimbaji wa makaburi wakiendelea na shughuli zao huku wakisisitiza kuwa maeneo yaliyobaki sio mengi.

Mmoja wa wachimbaji hao aliyeomba hifadhi ya jina lake, anasema maeneo ya makaburi bado yapo ingawa sio mengi kama ilivyokuwa awali.

"Kwa sababu sisi ni wazoefu wa uchimbaji wa makaburi hapa Sinza, tunayajua maeneo ambayo yamesalia ndani ya eneo hili. Hata sasa umetukuta tunaendelea kuchimba, hakujajaa," anasema.

Hata hivyo, ufuatiliaji wa Nipashe ulibaini kuwa kinachofanyika sasa kwenye eneo hilo ni kuchimba kaburi jipya kwenye eneo linalotenganisha kaburi moja na lingine.

Nipashe pia inatua mezani kwa Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, ambaye anakiri kujaa kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za maziko, lakini bado wanaendelea kuzika kwenye maeneo hayo hayo.

Anasema kwa sasa Jiji la Dar es Salaam linajipanga kutenga eneo jipya linaloandaliwa Kinyerezi ili kuongeza maeneo ya kuzikia jijini.

"Tunazika maeneo haya haya yaliyopo. Hivi sasa tunaandaa kiwanja kipatikane Kinyerezi kuongeza idadi ya maeneo ya kuzikia Ilala," anasema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwembe Madafu ulioko Ukonga jijini, Mbaraka Mohamed, anasema maeneo ya kuzikia ni yale yale ambayo ameyashuhudia tangu akiwa mtoto mdogo hadi sasa akiwa mtu mzima.

"Mimi ninachoamini makaburi huwa hayajai, tangu nizaliwe hadi hivi sasa mtu mzima makaburi ni yale yale. Kiimani sisi Waislamu makaburi hayajai, ila hivi sasa watu wanapozika kisha kujengea kwa saruji, zege wanafanya yajae haraka," analalamika.

Anasema eneo jipya sasa kwa ajili ya shughuli za maziko kwa wakazi wa Ukonga liko Mwanagati ambako kumeanza kutumika kutokana na kujaa kwa maeneo walikokuwa wanazika awali.

"Pia tulikuwa na makaburi ya Mzambarauni lakini sasa yamehamishwa kupisha ujenzi wa SGR (reli ya kisasa). Hapa kwa wakazi wa maeneo ya jirani kwa maana ya Ukonga, Mombasa, Madafu, Gongo la Moto utakuta wanakuja kuzikwa hapa kwa Zenje, Mombasa," anasema.

**WANAOZIKWA NA SERIKALI**

Si kila anayefariki dunia huzikwa na ndugu zake. Nipashe inazungumza na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, kujua mustakabari wa watu wanaofariki dunia huku kukikosekana ndugu wa kuchukua miili yao kwenda kuizika. Dk. Mfaume anasema Wizara ya Afya ngazi za mkoa wanaratibu maziko kwa watu wasio na ndugu lakini suala la wapi wazikwe, linashughulikiwa na maofisa mipango ya ardhi katika halmashauri.

"Suala la maeneo ya kuzikia wanaohusika ni maofisa ardhi wa halmashauri na ndio wenye taarifa zote. Idara ya Afya Mkoa tuna jukumu la kuratibu tu maziko ya watu," Dk. Mfaume anafafanua.

Nipashe Jumapili pia inazungumza na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura, ambaye anasema uandaaji wa maeneo ya kuzikia unaratibiwa ngazi ya mikoa na halmashauri ambao ndio wenye maeneo.

**Imeandikwa na Romana Mallya, Christina Mwakangale na Mary Geofrey.**



Sehemu ya makaburi ya Kisutu, eneo la Upanga, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ubalozi Pakistan wamlilia Geelani

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Pakistan nchini Tanzania, Mohammed Saleem, ameungana na watu wa Jammu na Kashmir kuombeleza kifo cha Syed Ali Shah Geelani akisema kifo chake ni pigo kubwa kwa dunia.

Geelani anajulikana kama baba na mwanaharakati wa kupigania uhuru wa Jimbo Kashmiri nchini Pakistan, alifariki dunia Septemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na Waandishi wa habari, Balozi Saleem alisema Geelani ataendelea kukumbukwa kwa harakati zake za kupigania uhuru wa Jimbo la Kashmiri.

Akielezea kifo cha Geelani, Mwenyekiti wa Kamati ya Kashmir hapa Tanzania, Ghazi Naeemullah amesema wanaombeleza kifo chake na kwamba kuondoka kwake ni pigo kubwa kwao.

"Najisikia huzuni sana hasa nikikumbuka harakati za Geelani katika kupigiania uhuru wa Jimbo la Kashmir kutoka India," alisema Neemullah.

"Geelani ni tochi ya maisha kwa wale wote waliokuwa wanapigania dekomorasia ya kweli," alisema.

Aliongeza kusema kwamba Geelani alionyesha mapenzi makubwa kwa watu wa Pakistan katika harakati za uhuru na amekuwa shujaa wa dunia na kifo chake ni pengo kubwa, lakini wataendelea kuenzi harakati zake.

Geelani alifariki dunia nyumbani kwake mjini Srinagar akiwa na umri wa miaka 92 baada ya kuugua kwa muda mrefu.

# Mamilioni wasotea vitambulisho NIDA

**Na Patson Andugalile,**
TUDARCo

OFISI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imesema ukaguzi wa ufanisi uliofanywa mwaka 2019/20 ulibaini asilimia 78 ya wananchi walioijiandikisha kupata vitambulisho vya taifa hawakuvipata kwa muda uliowekwa wa siku 180 tangu kujiandikisha.

Aidha, wako waliotumia miezi 18 yaani siku 563 kupata vitambulisho hivyo kutokana na kusuasua kwa uzalishaji kwa kile kilichoelezwa ni ubovu na kutotumika kwa mashine za uzalishaji kwa kiwango kilichotarajiwa.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkaguzi wa Ufanisi, Emmanuel Kisweka, wakati akiwasilisha mada ya ukaguzi wa ufanisi kwa wadau waliokuwa wanachambua toleo maalum la ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/2020.

"CAG anapendekeza kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapaswa kuwa na mikakati itakayowezesha wananchi wote wenye vigezo kupata Vitambulisho kwa wakati unaotarajiwa,"alisema.

Alisema lengo la ukaguzi lilikuwa ni kupima iwapo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia NIDA, imehakikisha Watanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi wamesajiliwa na kupewa vitambulisho vya taifa, ili kuboresha upatikanaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi, jambo ambalo lilionekana halikutimia.

Kwa mujibu wa Kisweka, lengo la ukaguzi wa ufanisi ni kutoa tathimini ya kiwango ambacho taasisi iliyokaguliwa inatumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi.

Pia uwekevu ni kupunguza gharama za rasilimali zinazotumika katika shughuli huku ukizingatia ubora stahiki, na ufanisi ni uhusiani kati ya matokeo na rasilimali zilizotumika kuzalisha au kuleta matokeo. Aidha, alisema tija ni kiwango cha kufikiwa kwa malengo na uhusiano kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi katika shughuli husika.



Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho (kulia), akizungumza na waliokuwa wakazi wa Magomeni Kota, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, na kuwahakikishia kuwa wote watarudi katika majengo mapya yaliojengwa na Serikali katika eneo hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uchaguzi mdogo udiwani Oktoba

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata sita za Tanzania Bara utakaofanyika Oktoba 9, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema jana kuwa sababu za kufanyika kwa uchaguzi huo ni madiwani husika kufariki na mmoja kukosa sifa ya uraia.

Alisema uchaguzi huo unafanyika baada ya NEC kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akiiarifu tume kuwapo kwa nafasi wazi katika kata hizo.

Dk. Mahera alizitaja kata hizo na wilaya zake kwenye mabano kuwa ni Kagera Nkanda (Kasulu), Kileo (Mwanga), Neruma (Bunda), Luduga (Wanging'ombe), Lyowa (Kalambo) na Vumilia (Urambo).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, fomu za uteuzi kwa wagombea zitaanza kutolewa Septemba 13 hadi 19, mwaka huu, uteuzi wa wagombea utafanyika Septemba 19, mwaka huu.

"Kampeni za uchaguzi zitaanza Septemba 20 hadi Oktoba 8, na upigaji kura utafanyika Oktoba 9, mwaka huu,"alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kashfa za ngono na ubakaji zimetia doa Polisi, Magereza

**WIKI** hii kumetokea taarifa mbili kuhusu majeshi ya polisi na magereza kuhusu baadhi ya askari wa vyombo hivyo kudaiwa kubaka, kulawiti na kuwalazimisha wanawake kingono pamoja na kuwanyanyasa kijinsia.

Taarifa ya kwanza ilihusu madai ya baadhi ya askari polisi katika wilaya ya handeni mkoani tanga kudaiwa kuvamia maeneo ya starehe, zikiwamo baa, nyakati za usiku na kuwataka wanawake kufanya nao ngono kwa lazima. Taarifa ya pili ni askari wa Jeshi la Magereza kutuhumiwa kumbaka na kumlawiti msichana.

Tukio la askari polisi kuwalazimisha wanawake kufanya ngono na kuwashika maungo, liliibuka baada ya Mkuu wa Wilaya (DC) ya Handeni, Siriel Mchembe, kupelekewa malalamiko na wananchi wa Kata ya Mdowe iliyoko Handeni mjini.

Baada ya kupata malalamiko hayo, mkuu huyo wa wilaya aliamua kufanya ziara katika eneo hilo akiwa ameongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, ambayo yeye ni mwenyekiti wake.

Wakati wa mkutano wake na wananchi wa eneo hilo, DC alielezwa kinagaubaga kwamba askari hao wakifika kwenye maeneo ya starehe, huwataka wanawake kingono na wanapokataa huwatafutia sababu na kuwakamata kisha kuwapeleka mahabusu.

Licha ya kuwalazimisha kingono, walidaiwa kuwa wanawachukua kwa nguvu wanawake na wasichana wakiwa na mabwana zao.

Kutokana na madai hayo, DC Mchembe alimwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ya Handeni kufanya uchunguzi lakini cha kushangaza Kamanda wa Polisi Mkoa (RPC) wa Tanga, Blasius Chatanda, ndani ya saa 48 tangu maagizo ya DC yatolewe, aliibuka na kukanusha madai hayo kuwa ni ya uzushi. Wakati RPC akikanusha, Jeshi la Polisi Makao Makuu limetoa taarifa kuwa limeunda timu ya uchunguzi juu ya tukio hilo.

Tuhuma hizo zimevitia doa vyombo hivyo vya ulinzi na usalama ambavyo vimepewa dhamana ya usalama wa raia na mali zao pamoja na kusimamia wafungwa ili kujirekebisha na kuwa raia wema mara wamalizapo vifungo vyao kwa wale wasio na vifungo vya maisha.


Pamoja na kutia doa vyombo hivyo, madai hayo ni mwendelezo wa yale ambayo yamekuwa yakizungumzwa juu ya vitendo vinavyofanywa na baadhi ya askari wa vyombo hivyo vikiwamo unyanyasaji wa raia kama vipigo, rushwa ya vitu na ngono na hata baadhi ya askari magereza kushiriki kutorosha wafungwa na kujihusisha na ngono na baadhi ya wafungwa na mahabusu.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alifungua mkutano wa maofisa wa Jeshi la Polisi huku akiwataka kujitathmini juu ya utendaji wao ikiwamo madai dhidi ya kuwapiga wahalifu na hata wengine kupoteza maisha, kubambikia watu kesi na kusuasua kwa upelelezi.

Mbali na Rais, wiki hii, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alilitaja Jeshi la Magereza kubadilika kiutendaji ikiwa pamoja na kuwahudumia wafungwa kama binadamu tofauti na mtindo wa kizamani wa mahabusu na wafungwa kulala sakafuni.

Kauli za viongozi hao ni dhahiri kwamba matendo maovu yanafanywa na baadhi ya askari wa vyombo hivyo. Kwa mantiki hiyo, kunatakiwa mabadiliko makubwa ili kutenda haki na kuendeshwa kwa weledi badala ya kuwa na dhana kwamba watuhumiwa na walioko makorokoroni wanapaswa kuadhibiwa au kutendewa kinyume cha ubinadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kunani idadi ndogo wanawake chanjo corona?

**KUFIKIA** Agosti 28, mwaka huu, watu 304, 603 walikuwa tayari wameshapata chanjo ya corona huku 201, 476 kati ya hao wakiwa wanaume ambao inaelezwa kuwa ni sawa na asilimia 66.1.

Wakati wanaume wakiwa kiasi hicho, kwa upande wa wanawake waliojitokeza kupata chanjo katika kipindi hicho cha mwezi mmoja tangu chanjo izinduliwe Julai 28 mwaka huu, walikuwa 103, 127, sawa na asilimia 33.9.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (anayeshughulikia Afya), Profesa Abel Makubi, wakati akitoa tathmini ya maendeleo ya chanjo hiyo iliyozinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika takwimu hizo, idadi ya wanawake inaonekana kuwa ndogo kuliko wanaume, hali ambayo inaonyesha kuwa huenda kuna jambo ambalo linachangia wasijitokeze kwa wingi.

Kwa nini kwenye chanjo ya kujikinga na corona wanawake wamekuwa nyuma? Ni kutokana na elimu potofu wanayopata mitaani? Hawajajua umuhimu wa chanjo? Au kwa sababu chanjo hiyo ni hiari?

Kila mwanamke huenda akawa na sababu zake zinazomfanya asiende kupata chanjo zikiwamo hizi ambazo zinatajwa na mratibu wa chanjo wa Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam, hasa kwa wale walioolewa.

Mratibu huyo Boniface Kitikila, anasema baadhi ya wanaume wanawazuia wake zao kwenda kupata chanjo, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inachangia kuwapo kwa idadi ndogo ya wanawake waliochanjwa.

Ni katika semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), anasema hayo kwamba amebaini kuwapo kwa hali hiyo kwenye manispaa yake, huku akishauri wenye mtindo huo kuacha ili wanawake wanaotaka kuchanjwa wapate huduma hiyo.

Mtindo huo unatajwa na watetezi wa haki za wanawake kuwa ni ukatili wa kijinsia kwenye chanjo, hivyo ingependekeza kama mtu angeachwa aamue mwenyewe kuchanjwa ama kutochanjwa kuliko kuzuiwa.

Ikumbukwe, serikali ilishaweka wazi kwamba chanjo ni hiari, hivyo inaweza kuwa ni kinyume na maelekezo ya serikali iwapo mtu atalazimishwa kuchanjwa au kuziwa kupata chanjo.

Kama kweli kuna wanaume wanawazuia wake zao kupata chanjo, watakuwa anapingana na watetezi wa haki za wanawake, ambao wanapiganía usawa wa kijinsia kwenye kila jambo.

Kwa kuwa chanjo ni hiari, anayemzuia mwingine asichanjwe au anayemlazimisha achanje, ninadhani wote kapu lao ni moja, ni vyema wakaelimishwa ili waachane na mtindo huo.

Uhai ni suala la mtu binafsi, hivyo si vibaya kila mmoja wetu akafanya sehemu yake kulingana na jinsi anavyotamani kulinda afya yake dhidi ya magonjwa mbalimbali badala ya kushurutishwa.

Binafsi ninaamini kwamba, serikali imetimiza wajibu wa kulinda raia wake kwa kuleta chanjo ili kwamba kila Mtanzania aliye tayari kuchanjwa, apate huduma hiyo bila kikwazo chochote.

Lakini wanapojitokeza baadhi ya watu na kuwazuia wengine wasichanjwe, ni kama hawawatakii afya njema, ndiyo maana watetezi wa haki za wanawake wanadai kwamba huo ni ukatili wa kijinsia.

Ingependeza iwapo wanaume wanaodaiwa kuwazuia wake zao wasichanjwe, wakatafakari kisha wachukue hatua sahihi za kuwaacha wawe huru kuamua hatima ya afya zao kuliko kulazimishwa.

Wanaowazuia wake zao kuchanjwa, wanaweza kujikuta katika kundi la wale wanaotoa taarifa za upotoshaji zisizothibitishwa na wataalamu wa afya na kuibua hofu na kusababisha kuwapo kwa idadi ndogo ya wanaochanjwa.

Ni vyema mambo yanayohusu wataalamu wa afya waachiwe wenyewe wayaseme, lakini pia ni vyema kila mtu aachwe aamue kuhusu usalama wa afya yake, kwa kuwa uhai ni suala la mtu binafsi.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Serikali iunge mkono juhudi za TradeMark East Africa



Pascal Mayalla

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema: "Tanzania itajengwa na Watanzania wenye moyo" na akaendelea kusema "ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora". Akaendelea kusema "fedha si msingi, fedha ni matokeo."

Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kuwa na hivyo vitu vyote alivyovisema Mwalimu. Watu tunao tele na wa kutosha, tunakaribia milioni 60. Ardhi tunayo ya kumwaga, kilomita za mraba, zaidi ya zenye ardhi safi eovu yenye rutuba, mvua zipo za kutosha, vyanzo vya maji lukuki, ardhi yenye rasilimali lukuki, kuanzia madini ya almasi, dhahabu, shaba, chuma, vito na sasa tuna gesi asili.

Pia karibuni tutagundua mafuta. Kwenye ardhi yetu tumebarikiwa kuwa vivutio vingi vya utalii, Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama, bahari, mito na maziwa. Kwa kifupi Tanzania tuna kila kitu.

Kwa upande wa siasa safi, mimi pia ni mjamaa na muumini wa Mwalimu katika falsafa ya Azimio la Arusha ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, japo Azimio la Arusha limeisha kufa na nafasi yake kuchukuliwa na Azimio la Zanzibar. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea imepigwa kumbo na mfumo wa soko huria, mfumo wa chama kimoja cha siasa umebadilishwa na sasa tuna vyama vingi.

Ukweli bado unabaki kuwa japo Tanzania tuna vyama vingi, kuikweli, kama ni vyama ni majina tu na kwenye makaratasi. Chama kama chama, Tanzania bado inatawaliwa na chama kimoja!

Nikimalizia hoja ya nne ya Mwalimu, uongozi bora, tunapoelekea kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanzania (Tangayika), siku zote tumekuwa na uongozi bora, toka Mwalimu mwenyewe, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa Samia Suluhu Hassan, wote hawa ni viongozi bora. Lakini tukilinganisha Tanzania mahali tulipo sasa na pale tulipopasa kuwepo, kiukweli tulipaswa kuwa mbali zaidi.

Bila kujiuliza tunakwama wapi, tutaendelea kupiga 'mark time' hapa hapa tulipo kwa mwendo wa jongoo kutokana na kuendelea kupanga bajeti tegemezi, mipango mkakati tegemezi, miradi mikubwa tegemezi, ambayo inategemea ama ufadhili, misaada au mikopo.

Maendeleo ya kweli endelevu, hayewezi kupatikana kwa kuendelea kuwategemea wafadhili, misaada na mikopo. Ili Tanzania tupate maendeleo ya kweli, lazima ijengwe na Watanzania wenye moyo. Vitu vyote hivyo vya kutuletea maendeo tunavyo sasa, tunakwama wapi?

Kwa maoni yangu, Tanzania tunakwama kwenye mambo mawili. Tunakosa kitu kinachoitwa 'SMART strategic objective', yaani malengo mkakati ambayo yako 'SMART'. SMART ni kifupi cha maneno 'Specific', 'Measurable', 'Attainable', 'Realistic' na 'Timely'. Ufafanuzi wake ni mada nyingine.

Pamoja na Tanzania kutokuwa na hizo 'SMART Objectves' katika mipango mikakati yetu kitaifa, inazo taasisi ningi zinazotumia huu mfumo wa 'SMART Objectves'. Moja ya taasisi hizo ni TradeMark East Africa. Kitu kinachofanywa na taasisi hii ya kinapaswa kuungwa mkono na si tu na serikali pekee, bali serikali zote za nchi za Afrika Mashariki na ikibidi serikali zote za bara la Afrika.

Kabla sijasema inachofanya, ni vizuri kwanza tuifahamu hii TradeMark East Africa ni nini? Malengo yake ni nini ndipo tuje kwenye inafanya nini. Tanzania tuko kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na tuko kwenye mchakato wa mtangamano wa Afrika Mashariki kuelekea kwenye shirikisho la kisiasa. Jambo hili linatekelezwa hatua kwa hatua, tumeanzia umoja wa forodha (customs union), tunakwenda soko la pamoja, tutakuja 'free labour movement', tutakuja umoja wa sarafu (monetary union) na kumalizia na shirikisho la kisiasa.

Japo binadamu wote ni sawa, watu wa nchi hizi hawafanani. Wengine ni wepesi wengine ni wazito. Miongoni mwa watu wazito katika kuchangamkia mambo ni sisi Watanzania!. Mfano mdogo ni huu wa chanjo ya corona. Watanzania tuko milioni 60 na wanaotakiwa kuchanja ni milioni 30. Tumepewa chanjo milioni moja za msaada nikidhani zingeisha ndani ya wiki moja lakini tunakwenda zaidi ya mwezi waliochanja hawajafika 500,000!

Wakati mchakato wa mtangamano unaendelea, Bara la Afrika limeingia kwenye mfumo wa soko huria kwa bara zima la Africa, AfCFTA, ambapo bidhaa za nchi zote Afrika zinaruhusiwa kufika nchi zote, hivyo Watanzania na bidhaa za Tanzania wasipojengewa uwezo, tulivyo wazito, tunaweza kujikuta nchi yetu ndio soko la bidhaa za wenzetu.

Sasa wanachofanya hawa TradeMark East Afrika ni kuboresha mazingira ya biashara kwa nchi za Afrika Mashariki na moja ya miradi yake ni kuwajengea uwezo wafanyabiashara wanawake ili bidhaa zao ziingie katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa.

Hivi karibuni, wakati wa Maonyesho ya SabaSaba, kupitia Chama cha Wafanyabiashara Wanawake wa Tanzania (TWCC), TradeMark East Africa, ilidhamini zaizi ya wanawake wafanyabiashara wa Tanzania 200, kuonyesha bidhaa zao baada ya kujengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo, utengenezaji wa bidhaa bora, vifungashio bora, kupatiwa nembo za ubora za TBS na 'barcode' na kupatiwa fursa za masoko ikiwemo kupelekwa hadi China. Sasa bidhaa za Tanzania zimeanza kupenya masoko ya Afika Mashariki na ya kimataifa.

Juhudi hizi za TradeMark zinatakiwa kuungwa mkono na serikali yetu. Hatuwezi kuendelea kuwategemea tu wafadhali kutuletea maendeleo, lazima nasi tuonyeshe moyo wa kujiletea maendeleo.

Badala ya TradeMark kuendelea kufadhiliwa na wafadhili na wahisani ili kuwasaidia Watanzania, serikali yetu nayo iweke mkono kwenye taasisi ili kazi nzuri za taasisi hizi ziwe endelevu. Ikitokea ufadhili wa wahisani umekwisha, kazi iendelee.

**0754 270403**
**pascomayalla@gmail.com**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tumetaga, tunaatamia, tutaangua Uviko!



Na Joseph Kulangwa

WATANZANIA naweza kusema wana usugu fulani ulioganda akilini mwao, unaowafanya wachukulie vitu au mambo kirahisi rahisi tu, kana kwamba hakuna baya limetokea na lipo.

Ama sivyo ni wepesi sana wa kusahau matatizo na kusonga mbele, huku wakijiaminisha kuwa Mungu yupo kuwasaidia kila kitu, maadam kawaumba basi hakuna siku watajitegemea.

Binadamu hawa wa Tanzania, siku zingine huwafananisha kama nyumbu walioko pale Serengeti ambao mmoja akiamua kufuata njia hii, wengine wote watafuata hata kama wa mbele atakumbwa na janga, watasimama kidogo na kufuata huko huko.

Ndiyo sababu ukiangalia mbashara, wanapovuka mto kila mwaka kuhamia upande wa pili kutafuta malisho na kwenda kutunga mimba, utaona wa mbele akidakwa na mamba na kugalagala, lakini wengine watapita hapo hapo na kugongana na mamba.

Nilipata kutabiri huko nyuma katika andiko fulani kuwa huenda katika miaka ijayo, tutakuja badilishana na wanyama, kwamba wao watakuja kuishi mijini sisi binadamu tuhamie mbugani, kwani akili zetu zinajiandaa kutuelekeza huko kabisa.

Angalia ni mwaka juzi na jana tu hapa alipoingia Uviko-19 nchini, akatupora pora ndugu na wapendwa wetu, tukahanikiza vilio wee, wakaja watu wakatuelekeza kupiga nyungu, kubwia mitangawizi na pilipili kichaa, changanya na vitunguu saumu na kadhalika.

Tukaona haitoshi, tukaambiwa tufunge tukiomba sambamba na kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni! Nani alikuwa anajua msamiati wa barakoa au maji tiririka? Nani alikuwa anajua vipukusi au sanitaiza, nani?

Kumbe Uviko akawa ametupanulia lugha yetu, tukazungumza mambo ya barakoa mpaka wakati mwingine ukawa kama utani vile, 'Bakari kabarikiwa kava barakoa, kaenda Barakuda', ukawa ni utani, lakini wenye elimu ndani yake, tukaendelea hivyo hivyo, ila tulipoona kiongozi hakuvaa barakoa nasi tukavua.

Tulidhani kiongozi huyo ndiye aliyetushikia akili na maisha yetu, kwamba asipokufa nasi hatufi, akifa tunakufa! Unyumbu wa aina yake ulikuwa ule.

Tukaambiwa na kijana mmoja wa chama fulani hivi, kwamba Uviko asipoishi nasi kwa nidhamu tutamtimulia mbali. Tukashangilia kinyumbunyumbu masikini sisi, huku tukiendelea kupukutika kama mbelewele.

Kipindi hicho wakaibuka wajasiriamali, kila mtu akawa mgunduzi wa dawa ya Uviko kwa ajili ya mwenzake, tukamkumbuka hata Babu wa Loliondo, aliyefanya yake mpaka akanunua magari na kujenga nyumba. Nyumbu sisi!

Viongozi wengine wakaona fursa ya kiki, wakaona sasa waonekane wanafanya kazi, wakajirekodi wakijifukiza kunako mablanketi, wengine wakajenga vibanda, vikafika mpaka kwenye hospitali kubwa zenye wataalamu wa afya. Shule tupa kule ingia kwenye mizizi ology. Nyumbunyumbu!

Kwamba tukasikia kuna chanjo imegundulika huko, tukaitamani ije na hapa kwetu tuokoe roho zetu na za wenzetu, wakati huo ambao hata kutaja tu kuna Uviko nchini ukawa mwiko, Uviko mwiko walahi! Usikike unasema fulani kafa kwa Uviko! Thubutu!

Nchi ikagubikwa na hofu, Uviko ikafutwa kwenye vichwa vyetu badala yake tukakubalika kusikika tukisema ni changamoto ya upumuaji, kwa kuwa Uviko alishaishi kwa nidhamu! Nyumbu kabisa walahi.

Alipoingia Mama Samia akasema lazima tukae chini tutafakari kwa kina, akaunda kamati ya kumshauri na kuangalia usalama wa chanjo, akaruhusu iingie. Akachanjwa.Tukachanjwa. He! Mara wakaibuka wajidhaniao wao ndio kumbe sio. Eti chanjo inasababisha uzombi!

Kiongozi wa Kanisa na kiongoziwa Chama Tawala, wakahanikiza kuwa hata aje nani, hakuna kuchanjwa, mwingine akaenda mbali akasema familia yangu (waumini wake) marufuku kujiunga na uzombi, chanjo imeletwa kwa wakuu wa nchi kuhongwa ili waue watu wao! Unyumbu wahed!

Haya tumechanjwa, ndiyo kwanza tunaitisha mikusanyiko mikuubwa kuelimishwa hatari ya mikusanyiko lakini na burudani. Mwananchi Day watu karibu 60,000 wakakusanyika Uwanja wa Mkapa, barakoa ngapi? Sijui.Haya Mbio za Mwenge wa Uhuru hizo zinakata mbuga. Mwenge anashika huyu anampa yule. Glovu wapi? Barakoa wapi? Maji tiririka je? Sabuni? Vipukusi?

Inashangaza kwenye mabasi ndiyo kabisaa, tunajiandaa na Mnyama Day! Tusijidanganye eti tumechanja basi kila kitu mukide. Tunataga, tutaatamia, tutasubiri kuangua

Vifaranga vya Uviko baadaye, tutakapokuwa tumeanza ligi na tumezima Mwenge.

**Alamsiki!**

KONA YA UKWELI

# Denmark kufunga ubalozi Tanzania ni jambo la kawaida, tusilete siasa



Na Thobias Mwanakatwe

KUMEKUWA na mjadala kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na uamuzi wa Denmark kufunga ubalozi hapa Tanzania ifikapo mwaka 2024, huku sababu zikitajwa kuwa ni kutokana na mpango wa nchi hiyo katika masuala ya kimataifa.

Mbali na Tanzania, nchi hiyo pia itafunga ubalozi wake Argentina, ubalozi mdogo wa Chongqing nchini China na ujumbe wa biashara huko Barcelona, Hispania.

Uamuzi huo ulitangazwa Agosti 27, mwaka huu 2021 na Waziri wa Mambo ya Nje wa Denmark, Jeppe Kofod. Alisema hayo ni matokeo ya sehemu ya marekebisho ya Denmark ya uwapo wa kimataifa ambayo yanajumuisha kuongezeka kwa ujumbe wa kidiplomasia uliopo na kufungwa kwa zingine.

Akasema upangaji upya unamaanisha uwakilishi zaidi utaboreshwa pamoja na mambo mengine, kazi ya Denmark katika mashirika na taasisi mbalimbali zikiwamo Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa mataifa (UN), Arctic na Afrika.

Alisema kipaumbele chake cha kwanza akiwa Waziri wa Mambo ya Nje ni kufunga ubalozi nchini Tanzania na kwamba hayo ni matokeo ya marekebisho ya vipaumbele vya serikali kwa ushirikiano wa maendeleo kama ilivyoainishwa katika mkakati mpya wa 'The World We Share'.

Mkakati huo mpya, alisema una msisitizo mkubwa katika kushughulikia udhaifu, nchi zilizo kwenye mizozo au changamoto za uhamaji na uhamiaji. Barani Afrika mwelekeo zaidi utakuwa Sahel na katika Pembe ya Afrika.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa Denmark itaheshimu ahadi zilizokubaliwa za kifedha na shughuli ya kufunga ubalozi imetengewa fungu ili kuhakikisha mchakato huo unakamilika vizuri.

Baada ya tamko hilo, serikali ya Tanzania nayo ilitoa taarifa ikieleza kusikitishwa na hatua ya Denmark kufunga shughuli za Ubalozi wake nchini. Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, katika taarifa take aliyoitoa Agosti 28, alisema hatua hiyo inasikitisha ikizingatiwa kuwa hivi karibuni serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikifanya jitihada za kufufua na kuimarisha diplomasia na uhusiano wa nchi rafiki, ikiwamo Denmark.

Kutokana na uamuzi huo wa Denmark, kumekuwa na mijadala mingi kwenye mitandao ya kijamii baadhi ya watu wakidai imechukuliwa kutokana na kuzorota kwa diplomasia katika kipindi cha mwaka 2016-2021.

Wakahoji kuwa Denmark ina balozi zake katika nchi tatu za Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Kenya na Uganda, hivyo uamuzi wa kuufunga ubalozi wake nchini ni kutokana na kuzorota kwa diplomasia. Wakaenda mbali zaidi kuwa eti Tanzania siku hizi tumekuwa tunawekwa kundi moja na Burundi, Zimbabwe, Korea Kaskazini Eritrea kwenye mambo kadhaa ya kimataifa.

Sikubaliani kabisa na watu wenye mawazo hayo kwamba diplomasia Tanzania imezorota ndiyo maana Denmark imefikia uamuzi huo. Wanaosema hivyo ni kwa sababu tu hawafahamu vizuri masuala ya kidiplomasia. Ni vizuri wakarudi darasani kujifunza ndipo waje na hoja zenye mashiko.

Watu lazima watambue kuwa suala la kufunga na kufungua ubalozi ni jambo la kawaida sana katika diplomasia. Ni sehemu ya maisha ya diplomasia. Diplomasia ina majira na misimu kama yalivyo maisha ya mwanadamu.

Mbaya ni kufunga uhusiano si kufunga Ubalozi. Denmark haijafunga uhusiano na Tanzania bali ubalozi. Huu ni utaratibu wa kawaida ambao unatokana na mazingatio ya siasa za ndani na maslahi ya kiuchumi ya nchi yenye ubalozi na si nchi mwenyeji.

Mifano ipo mingi. Tanzania iliwahi kufunga ubalozi Uholanzi na Sudan. Katika kipindi chote hicho, nchi hizo ziliendelea kuwa na balozi zao nchini. Hatimaye mwaka 2014 tukarudisha balozi zetu kwenye nchi hizo. Uhusiano na ushirikiano wetu haukufa kwa sababu ya kufungwa kwa balozi zetu kwenye nchi zao.

Tumewahi pia kuvunja uhusiano kabisa. Tulishavunja uhusiano na Uingereza, Ujerumani, Israel na Korea Kusini. Kote huko tumerejesha uhusiano na kurudisha balozi zetu. Leo tuna ubalozi Korea na Israel wakati Israel haijarejesha ubalozi wake Tanzania na wanawakilishwa kupitia ubalozi wao Nairobi.

Mifano hiyo inaonyesha kuwa kwanza si jambo la ajabu kwa Denmark kuamua kufunga ubalozi wake nchini. Pili, uamuzi huo ni matokeo ya siasa na maslahi ya kiuchumi ya nchini mwake zaidi kuliko Tanzania.

Wajibu wetu ni kuheshimu uamuzi wao, kuupokea, kuendelea kushirikiano nao na kuacha mlango wazi kwa wao kurudi mazingira na maslahi yao yakibadilika siku za usoni. Katika diplomasia hatujengi kuta, tunajenga na kuimarisha madaraja.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI DENMARK**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

DARASA LA NDOA

# Amani katika ndoa chachu ya maendeleo



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

TUNAISHI katika jamii inayobadilika na inayotupa wajibu wa kuendelea kukumbushana kuhusu suala la ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya taifa. Haki na amani ni mapacha wasiotengana.

Haki inahusika zaidi katika kuleta amani na uhusiano mzuri kati ya wanadamu, mwanadamu na uumbaji na kati ya mila, desturi na utamaduni. Hivyo, tunda la haki ni amani na mahali penye amani hutazamiwa kuwa na utulivu.

Kwa ujumla, haki ni suala mtambuka lenye kubeba mambo mengi. Kwa kutaja mambo machache; watu wana haki ya kuishi na kuwa na maisha mazuri yenye heshima na nidhamu; haki ya kulindwa katika maisha yao; haki ya kushiriki katika shughuli za maendeleo; haki ya kumwabudu Mungu kadiri ya imani na dhamira zao; haki ya kuchagua hali ya maisha wanayoyapenda zaidi haki ya kuchagua viongozi wanaowataka; haki ya kuwa huru katika kutafuta ukweli.

Ni jambo la msingi kufahamu kuwa siku zote haki huenda pamoja na wajibu na upendo. Haki pasipo upendo na kuwajibika ni unafiki na dalili ya kukaa ndani ya kifo. Amani ni moja ya matunda ya haki na zawadi kutoka kwa Mungu inayomwajibisha binadamu.

Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu na fungani ya binadamu. Hivyo, amani ni zawadi inayopaswa kutunzwa kwa njia ya kuwa na ndoa imara na malezi yenye dhamira nyofu kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa.

Watu wanapooa na kuolewa wajizatiti katika ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa. Wanandoa wafahamu nafasi na wajibu wao katika ndoa na kuepuka vitendo vya unyanyasaji na ukatili ndani ya ndoa. Wanandoa pia wanao wajibu wa kujifunza ili kufahamu misingi na madai ya taasisi ya ndoa kwa kuwa ndoa ni shule ambayo haina kuhitimu. Kila iitwapo leo ni siku ya kujifunza na kukua katika ndoa.

Kimsingi, jamii inatazamia kuona ndoa bora na si bora ndoa kwa kuwa ndoa ni msingi na kitovu cha malezi na familia. Ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia imara; familia zikiwa imara, tutakuwa na jamii imara; tukiwa na jamii imara, tutakuwa na taifa imara. Maendeleo ya taifa yanategemea uwapo wa ndoa imara kwa kuwa katika ndoa ndiko rasilimali watu inakotengenezwa. Watu ni rasilimali muhimu. Bila watu hakuna taifa wala maendeleo.

Ndoa zikiwa imara, haki, amani, utulivu na maendeleo vitaendelea kuwapo katika jamii. Umefika wakati sasa badala ya wazazi, ndugu na jamaa kujikita pekee katika kuandaa sherehe kubwa za harusi ni muhimu sana kuelekeza nguvu katika kuwaandaa vijana wa kike na kiume ili wawe wake na waume bora. Vinginevyo, tutakuwa tunaandaa sherehe kubwa za harusi za ndoa zisizodumu, hali inayoathiri mtu kisaikolojia, kiafya, kimwenendo, kiroho na kiuchumi. Athari hizi hasiwahusu vijana waliofunga ndoa tu, bali watoto waliozaliwa katika ndoa hizo na wazazi ambako wanandoa hao wanatoka.

Ni muhimu ikafahamika kuwa ndoa bora ni kielelezo cha hali ya juu kabisa cha upendo katika jamii; matunda ya ukomavu yanayohitajika katika ujenzi wa familia, uvumilivu, uaminifu na bidii. Kamwe tofauti za haiba (personality dynamics) kisiwe chanzo cha vurugu na mpasuko katika ndoa, kwani hali hii inaweza kuangamiza ustawi wa familia na maisha ya wanandoa wenyewe. Wanandoa wanapaswa kufahamiana vizuri, kuheshimiana na kuchukuliana katika tofauti na mapungufu waliyonayo ili kulinda utu, heshima na haki za binadamu.

Wazazi wamebeba dhamana kubwa ya malezi ya watoto wao. Wazazi wanao wajibu wa kulea watoto wao katika njia ipasayo na kuweka misingi bora ya maisha yao ya baadaye, kwani Wahenga wanasema, mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo. Wanasaikolojia wanasisitiza kuwa, zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya makuzi yake akiwa mtoto. Kwa hiyo, ili kutimiza wajibu wa malezi bora, wazazi wanapaswa kuwa kielelezo cha tabia njema na nidhamu.

Kutenda haki ili kutunza amani na utulivu katika ndoa ni wajibu wa kila mwanandoa. Hivyo, watu wanapoingia katika ndoa, mume na mke wafahamu kuwa wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa nyumba yao inakuwa kisiwa cha amani na utulivu na si kuwa uwanja wa fujo na visasi. Yote yatawezekana iwapo kila mwanandoa atatimiza wajibu wake na kumtanguliza Mungu.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

SEPTEMBA 5, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## RAHA YA MIHOGO SAMAKI



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Mambo muhimu ya kuzingatia kabla kupanga nyumba ya kuishi




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# JIPENDE KWA 'KNOTLESS'

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S | A | N | I | F | U |
| A | | | | I | |
| I | N | A | | K | |
| | U | | T | A | I |
| | K | | | | P |
| K | A | T | I | Z | O |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BIA, ZUA, PINDUA, MAISHA, ABIRIA, HUKUMU

## WATOTO

# PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa akilia baada ya kupigwa na wenzake wakati walipokuwa wakicheza mpira. Kaka yake alikuja haraka ili kujua nini kimemsibu.

Kaka: John unalia nini?

John: Kasim amenipiga baada ya kumwambia anipe mpira wangu

Kaka: Basi nyamaza twende nyumbani

John: Hapana mama akijua nimelia ataniadhibu

Kaka: Kwa nini?

John: Mama aliniambia shujaa huwa halii

Kaka: Hapana huo ni msemo tu, maana yake ni kuwa mvumilivu.

**SWALI**

Zao la Korosho linapatikana katika mikoa gani ya Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mbinu wanazotumia wenyeji kudhibiti wageni maeneo yao

KARIBU tena msomaji kwenye mwendelezo wa mada yetu kuhusu wenyeji na jinsi wanavyowapa wageni kashkash kwenye maeneo yao. Leo nitataja mbinu wanazotumia na jinsi ya kuwashinda.

Kwa wale waliobahatika kusoma makala iliyopita, nilijaribu kueleza vitisho vya wenyeji katika ardhi tunayoishi au kulima juu yake. Nikatoa ushuhuda wangu mwenyewe nikasema kwamba pamoja na vitisho vya kishirikina kwenye ardhi niliyonunua kwa mganga wa kienyeji, lakini mwishowe niliibuka mshindi.

Nilisema kuwa wenyeji au tunaweza kuwaita wenyeji wa nchi, ni wale watu waliotangulia kuwepo mahali fulani kabla yako. Wenyeji hawa ni wabaya kuliko unavyoweza kufikiria. Watu wengi hatma zao zimeuliwa na wenyeji wa maeneo wanayoishi pasipo kugundua.

Hakuna eneo lisilokuwa na wenyeji. Popote pale mtu alipo anatarajia awakute wenyeji hata kama yeye hawafahamu. Wenyeji utawakuta kwenye ukoo, shuleni, vyuoni, sehemu uliyopanga, sehemu ya biashara, maofisini na hata maeneo ya kilimo.

Mpenzi msomaji, hebu sasa tuangalie mbinu wanazotumia wenyeji kuvuruga maisha ya wageni katika maeneo yao. Ni ukweli usiopingika kwamba kila adui wa mtu hutumia mbinu ili kumshinda.

Tuangalie mbinu nne ambazo hutumiwa na wenyeji ili kuwashinda wageni. Kwanza, ni roho ya vitisho. Ni vema tukaelewa kwamba vitisho ni moja ya mbinu ambayo hutumiwa sana na wenyeji. Kumbuka kwamba watu hawa mara zote hawapendi kuzidiwa nguvu.

Kwa mantiki hiyo, kitu ambacho wanaweza kufanya ni kukutisha kwa maneno makali na kukufanyia vitendo vya kuogofya. Yote hiyo ni ili ukate tamaa. Watu wengi wangekuwa na mafanikio makubwa sana, lakini walijikuta wakiangukia mikononi mwa wenyeji na ndoto zao zikayeyuka. Vitisho humtoa mtu kwenye ndoto yake.

Unaweza ukawa unafanya jambo sahihi kabisa, lakini kama upo mikononi mwa wenyeji hutafika mbali. Wanasema, "tuwatishe ili waache kusema na watu hawa". Kwako wewe huenda wanasema, "tumtishe ili akimbie eneo hili. Endapo wewe ni jasiri lazima ukatae kutishwa kwa kusisitiza, "tutaendelea hatuwezi kuacha".

Mbinu nyingine ni roho ya kutojiamini. Mafanikio yoyote yanaletwa na mtu anayejiamini. Kukosa kujiamini siku zote kunamfanya mtu ashindwe kufanikiwa. Mwenyeji humfanya mtu ajione hajui lolote hata kama anajua. Hii ni mbinu inayowafanya wengi washindwe kujiamini. Msomaji wangu, uwe makini unapokuwa na mtu ambaye hakupongezi kwa kile unachokifanya. Wenyeji hutumia maneno kukufanya ujione dhaifu. Wengi hupoteza uwezo wa kujiamini kwa sababu ya maneno wanayotamkiwa na wenyeji wao. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Wapo watu wana uwezo mkubwa wa kufanya jambo, lakini kutokana na kukosa kujiamini wanaendelea kuwa chini ya wenyeji. Upo msemo kwamba, "jeshi la kondoo linaloongozwa na simba, litashinda jeshi la simba linaloongozwa na kondoo". Huu ni ukweli.

Hata kama una uwezo kiasi gani kama hujiamini uwezo huo hautakusaidia. Kumbuka mwenyeji hawezi kuguswa na kizuri ulicho nacho na siku zote hutaka atawale maisha yako.

Mbinu nyingine ni roho ya kuwa tegemezi. Wenyeji huwafanya wageni kuwa tegemezi. Hutengeneza mazingira uwategemee, uwanyenyekee na uwaogope. Mbinu nyingine ni kupuuzia mawazo yako hata kama ni mazuri.

Watu tuliowakuta kwenye maeneo ni mabingwa wa kuua mawazo ya wageni. Utatoa wazo zuri lakini atalipuuzia. Hii ni kujaribu kukuonyesha wewe hujui. Mbinu nyingine ni kuzindika akili za wageni ili wasigundue hila zao ovu.

Wenyeji wengi hawana maendeleo katika miji au maeneo wanayokalia. Wageni wanapokuja huzindika akili zao ili wafanane nao. Hizo ni roho zinazokulazimisha uishi kama wao.

Msomaji wangu tumalizie kwa kuona jinsi ya kuwashinda wenyeji. Ili kuwashinda, ni muhimu sana ukaweka agano la maombi na Mungu. Vita dhidi ya wenyeji inahitaji mwendelezo wa maombi.

Isitoshe, yapo mambo ya msingi ya kuzingatia. Kwanza ni lazima uwe mvumilivu. Watu wanaopata ushindi mkubwa ni wale wanaovumilia. Vinginevyo ushindi kwao ni ndoto.

Vile vile ni lazima uwe mtu wa kutunza siri zako kwa wenyeji. Usiwaambie mambo yako. Pia lazima uwe jasiri. Ni dhahiri kwamba ujasiri hutupatia thawabu kuu. Usitarajie kuwa na thawabu kama ujasiri umeutupa mbali nawe.

**Niishie hapa na bila shaka mada hizi zimekuelimisha. Je, una maoni au kisa cha maisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581 .**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Maegesho hospitalini, nyumba za ibada yaangaliwe

SEPTEMBA Mosi, mwaka huu, umeanza kutumika utaratibu mpya wa kukusanya tozo za maegesho katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam. Kupitia utaratibu huo, mtu anatakiwa kulipa kwa simu au benki kupitia namna maalum ya malipo 'control number'.

Utaratibu wa awali ulikuwa wakusanyaji kupewa fedha taslimu baada ya kukuwekea stakabadhi ya madai kwenye gari lako, ambao unadaiwa haukuwa na ufanisi kwa kuwa fedha za umma zilipotea.

Napongeza utaratibu huu kwa sababu serikali itakusanya fedha zote kwa usahihi, ingawa kwa upande mwingine unamuumiza mmiliki wa gari kwa kuwa gharama za kutuma hiyo fedha zinaongezeka.

Maumivu yapo. Iwapo atatuma kwa kutumia simu atakutana na makato ya tozo ya miamala na kampuni za simu, na ikiwa ataamua kulipia kwa wakala au benki maana yake anatakiwa kutumia muda.

Kwa mujibu wa utaratibu huo mpya, iwapo mmiliki wa gari hatalipa tozo hiyo ndani ya siku saba, atatakiwa kulipa mara mbili na zikipita siku 14 atafikishwa mahakamani na akikutwa na hatia, atatakiwa kulipa faini ya Sh. 300,000 au kifungo cha miezi 12 jela. Ikiwa atakiri kosa basi atalipa Sh.30, 000.

Kwa sasa mtu akikutwa ameegesha gari pasipostahili (wrong parking) anatakiwa kulipa faini ya Sh.30, 000.

Kwa ujumla, lengo la utaratibu huu mbali ya kwamba ni kukusanya mapato lakini ni kuhakikisha kuna utaratibu mzuri wa kuegesha magari maeneo ya miji ili kuondoa usumbufu au kuwa kama uchafu.

Pamoja na nia njema iliyopo bado kuna suala ambalo ni lazima Wakala wa Barabaza za Vijijini na Mijini (TARURA), ikaliangalia kwa jicho la pekee ambalo ni kukusanya maegesho katika meneo ya huduma muhimu za kijamii kama hospitali na nyumba za ibada.

Kwa sasa utaratibu uliopo wanakusanya fedha za maegesho kila mahali ikiwamo kwenye nyumba za ibada na hospitalini ambako watu wanakwenda kupata huduma muhimu za kijamii.

Mathalani, kwa Waislamu huenda ibadani mara tano kwa siku, yaani asubuhi, adhuhuri, alasri, magharibi na Isha, kati ya hizo tatu lazima zitamkuta katika muda wa maegesho ambao wakusanyaji wapo na wataweka stakabadhi na kuondoka. Maana yake mtu anayekwenda kuswali msikitini kama ana gari, kila siku aandae Sh. 1,500 ya kulipa na ikiwa atachelewa itakuwa Sh. 3,000. Kwa Mkristo anayekwenda kanisani kwa nyakati tofauti naye anapaswa kutenga kiasi hicho cha fedha.

Kwa mujibu wa utaratibu, muda wa kutoza maegesho huisha saa 11:00 jioni lakini wapo wanaoendelea kusubiri hadi usiku na baadhi wamegeuza ndiyo namna ya kujipatia fedha. Maeneo kama Mwenge na Kariakoo, kuna huu mchezo wa kulazimisha wenye magari kutoa fedha na huwa wana stakabadhi kabisa.

Kwa anayekwenda hospitalini, anatakiwa kuandaa wastani wa Sh. 2,000 kwa kuwa anaweza kutumia muda mwingi kutokana na foleni au kusubiri majibu ya maabara ambayo hutegemea aina ya kipimo.

Mathalani, hivi karibuni nilikwenda katika hospitali moja Dar es Salaam kuanzia saa 4:00 asubuhi na nilitoka saa 12:00 jioni. Kutokana na taratibu za kupata majibu ya maabara na kumwona daktari na kukuta bili ya maegesho ya Sh. 4,000 ambayo nililipa, nilijiuliza ikiwa nilikwenda katika eneo hilo si kwa kupenda au kutafuta kipato bali kwa ajili ya kupata matibabu na kama natibiwa kwa fedha taslimu maana yake napaswa kujipanga kugharamia vitu vyote hivyo.

Ziko Hospitali nyingi za siku nyingi ambazo hazina maeneo ya maegesho na watu wanaopeleka ndugu zao au wanapokwenda wenyewe kwa ajili ya matibabu, wanapaswa kuandaa fedha ya ziada ya kugharamia maegesho.

Pia unapokwenda kuona mgonjwa asubuhi, mchana na jioni na ukawa umetumia gari na kuliegesha eneo hilo, basi unapaswa kuwa na fedha ya kulipa maegesho kwa muda wote huo na kama mgonjwa wako atakaa mwezi mmoja maana yake utatakiwa kulipa fedha nyingi zaidi.

Eneo lingine ni kwenye vyuo na shule, napo siku hizi kunatozwa maegesho kiasi ambacho ni maumivu kwa wazazi ambao huwarahisishia watoto wao kuwa na usafiri.

Kwa ujumla ni muhimu utaratibu huu ukaangaliwa upya kwamba katika maeneo ya hospitali na nyumba za ibada kuwe na tozo ndogo kuliko maeneo mengine ya ofisi au shughuli nyingine, ni muhimu kujua kuwa wanaokwenda kwenye maeneo hayo wanalazimika kwenda na siyo kwa kupenda na haifai kabisa kuwatoza.

Inawezaka kabisa kuzitambua hospitali ambazo hazina maeneo ya maegesho na kusaidia kuwapo utaratibu mzuri wa kuhakikisha hakuna maumivu makubwa.

Hakuna ubishi kwamba ni muhimu kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi, lakini isiwe kwamba ukishamiliki gari basi unakuwa na kodi nyingi ambazo kwa wakati mwingine ni maumivu.



ILIKUWA NI SIKU YA FURAHA KWA HEMED YASIN, ALIPOFUNGA NDOA NA JOYCE HERMAN KATIKA UKUMBI WA NEW TAIFA, TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM, OCTOBA 27, 2019.









# MITINDO

Na Christina Mwakangale



# 'KIGODORO' VAZI TATA
## Lakini linaongeza vionjo

DUNIA inakwenda kwa kasi na mitindo ya maisha inabadilika kila wakati kulingana na mahitaji ya watu ya wakati husika.

Vazi la 'Kigodoro' limepata umaarufu kwa wanawake wengi kutokana na umuhimu wake wa kuongeza mwonekano wa umbo kwa baadhi ya watu.

Kigodoro ni aina ya vazi ambalo hutumika na wanawake kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa makalio na mapaja, hii humfanya mvaaji kuwa na umbo lililokatika vyema hata kama ameumbwa kawaida.

Vazi hili hutengenezwa kama kaptula, lakini huongezwa na vitu kama sponji sehemu ya nyuma au pembeni maeneo ya mapaja.

Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, wabunifu wanabuni na kutengeneza aina tofauti ya vigodoro ambavyo vinawafanya watumiaji kuvutiwa na kununua.

Matumizi ya nguo hizi huvaliwa sana wakati wa sherehe mbalimbali kama harusi ambako wanawake wanataka kujionyesha upekee wao. Pia wengine huvaa wakati akienda kazini au matembezi ya usiku.

Hata hivyo, kumekuwa na mawazo tofauti kuhusu matumizi ya vazi hilo, wapo wanaunga mkono kwamba ni sehemu ya mavazi ya kawaida kwa mwanamke, lakini kuna wanaopinga na kusema linaharibu mtazamo mzima wa mtu na kushindwa kujiamini.

## UREMBO

Na Mary Geofrey



# JIPENDE KWA 'KNOTLESS'

UZURI wa mwanamke hupambwa zaidi na usafi wa kichwa chake na aina ya mtindo wa nywele alizosuka.

Wanawake wengi hupendelea kubadili mitindo ya nywele ili kuendana na wakati.

Katika siku za karibuni wanawake wengi ndani na nje ya Tanzania wamekuwa wakisuka mtindo mpya wa rasta za mabutu, maarufu kama Knotless.

Mtindo huu wa nywele umebamba kwa wanawake wengi na kuwafanya waonekane wenye mvuto.

Usukaji wa nywele hizi ni rahisi, hutumia muda mfupi na haziumizi kichwa kama ilivyo kwa mitindo mingine ya vitunguu kama vya kunyonga chini.

Usukaji wa nywele hizi pia hutumia muda mfupi na huziacha nywele kuwa salama wakati wote.

Wasusi wa nywele hizi huona ni kazi rahisi zaidi ukilinganisha na misuko mingine kwa sababu hauhitaji kutumia ubunifu zaidi ya kukata mistari iliyolingana.

Wanawake wanaosuka nywele hizi pia hubaki kuwa watanashati kwa muda wa wiki mbili na zaidi kabla ya kuanza kuchoka.

Wengine huanza kuchoka kuanzia mwezi mmoja kulingana na matunzo na kichwa cha mtu kama hakiwashi.

Ukisuka nywele hizi unaweza pia kubana kwa mitindo tofauti kama kidoti, upande na staili ya kuzirudisha nyuma.

Unaweza pia kuziachia kama unaenda kwenye shughuli yoyote au mtoko wa weekend itapendeza zaidi na kuendelea kubadili mwonekano wako.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# RAHA YA MIHOGO SAMAKI

CHAKULA ni muhimu kwa maisha ya binadamu na kinanoga zaidi kama kikipikwa vyema.

Mihogo ni chakula kizuri ingawa imezoeleka kupikwa kama kitafunwa kwa kukaangwa au kuchemsha.

Wapo wanaopika mihogo kwa kuiunga na nazi na kuliwa kama futari kwa wanaofunga kwa ajili ya kula jioni.

Leo katika safu hii tunaelimishana namna ya kupika mihogo kama mlo kamili wa mchana au usiku na mboga zake nzuri za samaki na maharagwe.

Mahitaji

Kitunguu maji, pilipili manga, mihogo vipande viwili vikubwa, mafuta ya kupikia, limao au ndimu, pilipili manga ya unga na nyanya mbili.

Namna ya kuandaa

Anza kuandaa samaki kwa kuwaosha vizuri na kumkata vipande na kisha unyunyuzie limao au ndimu, weka chumvi, tangawizi, pilipili manga na viungo vingine upendavyo kwenye samaki.

Hifadhi samaki pembeni au kwenye jokofu kwa muda ili viungo viingie vizuri kwa dakika 15.

Menya mihogo, osha na kata vipande vidogo ili iwe rahisi kuiva na kisha andaa maharagwe yaliyoiva tayari.

Pika mchuzi wa nyanya ambao unaweza kuweka pia kipande cha samaki ili kuongeza ladha.

Anza kuchemsha mihogo kwenye kikaangio au sufuria hadi iive na kulainika vizuri.

Unaweza kuandaa kachumbari ya nyanya, tango na karoti kama unapendelea tayari kwa ajili ya kula mlo wako.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Mambo muhimu ya kuzingatia kabla kupanga nyumba ya kuishi

## Dondoo za kuchagua zulia kwenye sebule



PAMOJA na kuwa matumizi mazulia yamepungua kutokana na uwepo wa teknolojia ya marumaru, lakini pambo hilo ndani ya nyumba linabaki kuwa muhimu.
Katika kuhakikisha nyumba yako inakuwa maridadi kwa kuweka zulia safi kwenye sebule, hizi ni baadhi ya dondoo zitakazokufanya kuwa na chaguo zuri.

1. Hakikisha unachagua zulia lenye rangi inayofanana na baadhi ya vitu vyako vya ndani.

2. Kabla ya kununua, unapaswa kuamua juu ya vipimo sahihi, mapambo na michoro.

3. Unapaswa pia kuzingatia urefu wa zulia, haipaswi kuwa ndefu sana kwenye sebule.

4: Chagua aina ya zulia unalopenda kulingana na malighafi iliyotengenezwa, zulia laini linapendeza kuwekwa sebuleni kwa sababu halimchoshi mtu akikaa chini.

YAKO mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kupanga nyumba ya kuishi.

Kufahamu mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kulipia nyumba na kuanza kuishi kuna faida zake. Baadhi ya mambo tunayoangalia leo katika ukurasa wetu huu ni pamoja na eneo nyumba ilipo na umbali.

Kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi, lakini ikawa mbali zaidi au ikakulazimu kutumia pesa zaidi kwa upande wa usafiri.

Huenda kama unatumia usafiri wa umma, ikakulazimu kila ukifika kituoni utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo. Kwa hiyo ni lazima ufikirie kwa makini kabla ya kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo la sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba zinaonekana vizuri kwa nje, lakini ndani zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea.


Kwa hiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe.

Lingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba, hawasemi ukweli na badala yake baada ya kulipia na kuanza kuishi ndipo huanza kuyasema kidogo kidogo kwa wapangaji, hivyo ni vyema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.

Kusoma kwa makini mkataba kabla ya kulipia pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya, lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia na mkataba wako unausoma vizuri na kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza, anafanya hivyo kama ilivyo kwako na kama utabaini kuna kitu kinakufunga ni bora uulize mapema kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
SALIO LAKO LA KUISHI KWA AMANI LINAZIDI KUANGAMIA JIANDAE KUNIAMKIA BWA'MDOGO
MIMI HAPA KWANGU SIRUHUSU MIPASHO, SUBIRI AU KAUNGANE NA AKINA MASHAUZI
MIMI NAMPA LIFTI YULE MPANGAJI WA KIKE ILI ASISUKUMWE KWENYE MADALADALA...
NA MIMI NAONGOZANA NA YULE MPANGAJI WA KIUME ILI ASISUMBULIWE NA VISICHANA
MSHENGA SIKUELEWI TOKA UPELEKE BARUA YANGU NAKUONA TU!
BARUA ZIMEGONGANA NYINGI NDIO WANATAKA KUCHEZESHA DROO YA BAHATI NASIBU...
KAMA KWELI NI MJOMBA WAKO MBONA YEYE ANA PUA KUBWA KAMA ANAFUA UPEPO?
ILE NI YA URITHI WAKATI WA KUGAWA MIRATHI YEYE NDIO KAAMBULIA ILE...
MBONA YEYE KAFANANA NA HAYATI 'PEPE KALE' KWANI NDUGUYE?
KAMA MKE WA MTU NI MZURI, NGOJA WENZAKO WAKUBEBEE WAKO UONE... USIKODOLEE MADENTI SKETI YA SHULE HATA MKEO INAMPENDEZA KAMSHONEEEEE...
JANA TULIKUNYWA NIKAANGUSHA GARI BAR, TULIKUWA MIMI NA WEWE... WAIFU KAJUAJE?
KWANI MDOMO SINA?
KAMA KWELI UNANI-PENDA... TUONGELEE UMUHIMU WA AFYA ZETU KWANZA...
ANAKOELEKEA TUKACHANJE NA KUPIMA VIRUSI... 'KILANGA KOMO!'
MGANGA HANIDAI CHOCHOTE NAMLIPA KWA WAKATI
MWAKA UMEKATIKA KODI YA NYUMBA UJA-LIPA MGANGA ANA-MSAHAULISHA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KUTELEZA SI KUANGUKA...KISHUKURU KISIGINO

HABARI KIMATAIFA

# Mapigano makali yaendelea kuwania Bonde hatari la Panjshir Afghanistan

**KABUL, Afghanistan**

MAPAMBANO kati ya Taliban na vikosi vya upinzani yameongezeka katika kuudhibiti mkoa wa kaskazini wa Panjshir.

Panjshir ambayo inazungukwa na milima mikali, limekuwa eneo hatari na ni vigumu kwa vikosi vya kijeshi kuingia kwa urahisi kuudhibiti.

Mamia ya familia zimekimbia, wakati Taliban ikipambana kuchukuwa udhibiti wa ngome hiyo ya mwisho ya waasi.

Wakazi wa maeneo jirani ya Mkoa wa Parwan wanasema kwa siku nne sasa maisha yao yamevurugwa na mapigano yaliopamba moto kati ya Taliban na vikosi vinavyoongozwa na Ahmad Massoud, mtoto wa kamanda alieuawa, Ahmad Shah Massoud.

Viongozi wa Taliban walisema juhudi za kufikia mwafaka kwa njia ya majadiliano zilishindwa kuzaa matunda, wakati kundi hilo likijiandaa kutangaza kuundwa kwa serikali mpya, wiki kadhaa tangu kutwaa madaraka.

"Mapigano yamekuwa mabaya zaidi kila usiku," alisema mkaazi wa mji wa Jab al-Seraj Asadullah mwenye umri wa miaka 52.

Wakazi hao walisema mapigano yalioongezeka yamezilazimu familia zisizopungua 400 kukimbia vijiji vilivyoko kwenye barabara ambayo kawaida inaelekea kwenye mabonde tulivu na ya kijani ya Panjshir umbali wa karibu kilomita 125 kaskazini mwa mji mkuu Kabul.

Moshi ulionekana ukitanda kutokea milima ya mbali wakati Wataliban wakipigana kutaka kudhibiti mkoa wa mwisho kati ya mikoa 34 ya nchi hiyo.

Walionekana wanajeshi wa zamani wa jeshi la taifa la Afghanistan kutoka mikoa wa Kunduz, Kapisa, Parwan na Takhar wakielekea Panjshir baada ya mikoa hiyo kuangukia kwa Taliban.

Mashuhuda walisema wanajeshi hao walikuwa wanasafirisha magari ya kijeshi na vifaa vingine.

Hata hivyo, kulikuwa na taarifa chache kwenda na kutoka Panjshir, ni vigumu kuhakiki madai hayo au kujua ni kiasi gani cha zana hizo zimetumiwa katika siku za hivi karibuni.

Siku ya Ijumaa usiku kulisikika milio ya risasi mjini Kabul, kusherehekea ushindi kufuatia uvumi kwamba bonde la Panjshir limeangukia mikononi mwa Taliban, lakini Wataliban hawakutoa taarifa yoyote rasmi. Wapiganaji kutoka National Resistance Front, kundi linaloundwa na wanamgambo wanaoipinga Taliban na vikosi vya zamani vya usalama vya Afghanistan, wanaaminika kuwa na akiba kubwa ya silaha katika bonde hilo, ambalo liko karibu kilomita 80 kaskazini mwa Kabul. Ali Maisam Nazary, msemaji wa kundi hilo, alidai kuwa mapigano yalikuwa makali na kwamba wanapambana kulinda eneo lao.

Wakati huo huo, Umoja wa Mataifa utafanya mkutano kujadili misaada ya kimataifa mapema mwezi huu mjini Geneva.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonia Guterres, aliielezea hatua hiyo inalenga kuepusha janga la kibinadamu linalojitokeza nchini humo.

Guterres alitoa tangazo hilo kupitia ukurasa wa Twitter akiitaka Jumuiya ya kimataifa kushirikiana katika kuwasaidia Waafghanistan.

Aidha mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa ametoa wito wa upatikanaji wa misaada na kuhakikisha raia wa

nchi hiyo wanaendelea kupata huduma muhimu wanazohitaji. Mashirika ya misaada ya kiutu yalisema awali kuwa, raia wengi wa Afghanistan walikuwa tayari wanakabiliwa na changamoto ya kuzilisha familia zao katikati mwa ukame uliokithiri kabla ya Taliban kuchukua udhibiti.

Kuna wasiwasi kuwa wananchi wengi huenda wakakabiliwa na njaa kutokana na nchi kutengwa na uchumi kuzorota. **DW**



Wapiganaji wa kundi la Taliban wakiwa katika lango la kuingia Mkoa wa Panjshir ambako kumeripotiwa kuwapo mapigano makali na wanamgambo wenye msimamo mkali. **(PICHA: DW)**

# Marekani kuweka wazi shambulio Sept 11

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ametoa agizo la kuwekwa wazi baadhi ya nyaraka zinazohusiana na mashambulizi ya kigaidi ya Septemba 11, mwaka 2001.

Alisema hatua hiyo ni ya kuziunga mkono familia za wahanga, ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikitafuta rekodi hizo kwa matumaini ya kuishtaki serikali ya Saudi Arabia.

Agizo hilo lililotolewa kabla ya kumbukumbu ya miaka 20 tangu kutokea mashambulizi hayo, ni muhimu katika mvutano wa miaka kadhaa kati ya serikali na familia hizo, kuhusiana na taarifa zipi za siri zinaweza kuwekwa wazi. Ndugu wa waliofariki, waathirika na maofisa wa uokozi walipinga ushiriki wa Biden katika matukio ya kumbukumbu ya Septemba 11, ikiwa nyaraka hizo zitabakia kuwa siri.

Kesi ya muda mrefu katika mahakama ya shirikisho mjini New York inalenga kuiwajibisha Saudi Arabia na inadai kuwa maofisa wa nchi hiyo waliwasaidia watekaji kabla ya mashambulizi hayo. **DW**

**Agizo hilo lililotolewa kabla ya kumbukumbu ya miaka 20 tangu kutokea mashambulizi hayo, ni muhimu katika mvutano wa miaka kadhaa kati ya serikali na familia hizo, kuhusiana na taarifa zipi za siri zinaweza kuwekwa wazi. Ndugu wa waliofariki, waathirika na maofisa wa uokozi walipinga ushiriki wa Biden katika matukio ya kumbukumbu ya Septemba 11, ikiwa nyaraka hizo zitabakia kuwa siri.**

# Serikali, wapinzani kuijadili Venezuela

**MEXICO CITY, Mexico**

SERIKALI ya Venezuela na upinzani wamerejea katika meza ya mazungumzo yanayofanyika nchini Mexico.

Wapinzani wanataka uchaguzi huru na haki, huku upande wa Rais Nicolas Maduro, ukidai kuondolewa vikwazo. Muungano mkuu wa upinzani ulitangaza wiki hii kuwa utashiriki tena uchaguzi wa manispaa mnamo mwezi Novemba, baada ya kususia kwa miaka mitatu.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya pande hizo mbili kuanza mazungumzo mwezi uliopita, yakiratibiwa na Norway na mwenyeji Mexico, katika juhudi za kuutafutia ufumbuzi mgogoro wa kisiasa ambao umegubika utawala wa miaka nane ya Maduro.

Mazungumzo hayo yana vipengele saba ikiwamo kulegezwa kwa vikwazo, haki za kisiasa na uchaguzi lakini sio kuondoka kwa Maduro ambaye anatuhumiwa na upinzani kwa udaganyifu katika uchaguzi wa 2018.

## MAKALA



Na Magabilo Masambu

# UONGOZI NI MATENDO SI MANENO

MAISHA binafsi ya kiongozi wa kweli katika matendo, hayana budi kuakisi maisha halisi ya wale anaowaongoza na hupaswa kuwa nao katika hali zote. Iwe ni katika hali ya neema au taabu na shida. Yeye hupaswa kuwa mwongozo wao juu ya kutatua matatizo yanayowasibu watu kwa wakati huo bila kuwakimbia.

Watu ni rahisi sana kujifunza kwa vitendo zaidi kuliko maneno. Maisha pekee ya kiongozi yanaweza kubadilisha maisha ya watu wake. Mfano, kama kiongozi ataishi maisha ya starehe, wananchi watajifunza aina hiyo ya maisha. Hawatakuwa watu wa kufanya kazi.

Kama wote tunakubaliana kwamba nchi zetu ni maskini, basi umaskini huo haupaswi kuonekana tu kwa wananchi wanaoongozwa, bali unapaswa kuonekana hata kwa viongozi wetu. Kama ni utajiri uonekane kwa wote pia. Lakini tujiulize je, ni kweli maisha ya viongozi wetu yanafanana na maisha ya wananchi wao?

Hatuwezi kuendelea kusema tu midomoni kuwa sisi ni wazalendo, wakati matendo yetu hayathibitishi matamshi yetu. Kitendo cha viongozi wetu kujipatia huduma bora zaidi katika taasisi binafsi, wakati wao ndio wenye dhamana ya kuimarisha taasisi za umma, hakitofautiani kabisa na baba anayeikimbia familia yake wakati wa shida.

Viongozi tukibadili aina ya mfumo wa maisha yetu binafsi badala ya kutumia rasilimali za taifa kwa wachache, zikatumika kuwahudumia watu wote nchini. Ili kupata huduma bora za kijamii kama afya, elimu bora pamoja na makazi ya uhakika tutatengeneza watu wema sana hasa katika kulipa kodi. Lakini kutokana na aina ya maisha ya viongozi wetu kwa leo, kila mtu anatamani awe mwanasiasa maana anajua akishakuwa mwanasiasa tu tayari atakuwa tajiri. Siasa zimegeuka vita.

Kwa hiyo si kwamba watu wetu wamekuwa na ufahamu mkubwa sana juu ya siasa bali ni kutokana na kuona maisha wanayoishi viongozi wetu wa kisiasa ambao ndio wasimamizi wakuu wa rasilimali za taifa.

Tunao mfano wa Mwalimu Julius Kambarage yerere aliyekaa Ikulu kwa muda wa miaka 24 lakini kila mtu anaweza kueleza kuwa maisha aliyoishi hayakuwa ya anasa kama tunavyoona kwa baadhi ya viongozi wetu leo! Nyerere ni kiongozi aliyekonda kwa matatizo ya wananchi wake.

Natambua, amefanya mengi kupitia maisha yake binafsi kubwa likiwa ni la kutufanya Watanzania leo tuishi bila kuulizana makabila yetu japo kila mmoja ana kabila lake. Kuna wakati hata wanaotupatia misaada hutushangaa sana, tunaopatiwa misaada tunaishi maisha ya anasa zaidi makazi ya maana kuliko hata ya watoa misaada.

Lakini inawezekana hata ombaomba barabarani akawa na maisha mazuri kuliko mwalimu au askari kwa sababu akaapo barabarani hupita watu wenye uwezo tofauti na ombaomba yule ili aendelee kupata fedha zaidi ni sharti aendelee kukaa pale katika mazingira ya kimaskini ili apate misaada mingi zaidi.

Tabia hii ya kuendelea kwenda mikono nyuma kuomba misaada kwa wakubwa na tukishapata misaada hiyo tunaishi maisha ya anasa ni kujidhalilisha na kuudhalilisha utu wetu. Misaada hiyo ingetumika kwa usahihi ili kujenga misingi imara ya uchumi wa nchi zetu na baada ya muda tusiwe ombaomba tena.

Binafsi, niliwahi kuvua na kuloa samaki katika Ziwa Victoria nilipokuwa naishi kijijini Bulenda Bufwe. Tabia ya wavuvi moja kubwa ni kwamba akienda kuvua samaki na akapata anaporudi nyumbani, huuza samaki wote wazuri na kubakiza samaki wachache tu wa ovyo kwa ajili ya kitoweo cha familia yake.

Samaki wote hao hupikwa na kuliwa wote maana huamini jioni yake atarudi na kupata samaki wengine. Wale aliowauza ile pesa anaishia kunywea pombe. Jioni yake huenda tena ziwani kwa ajili ya kuvua au kuloa tena na hayo ndiyo maisha ya mvuvi kila kukicha.

Kwa upande wa pili, wako watu ambao kazi yao huenda kila siku kuomba samaki kwa wavuvi na hii ni kwa sababu hawajui kuvua. Tukumbuke kuwa samaki wa kuomba huwezi kufanyia biashara kwa maana ya kuwauza ili upate fedha. Kwa hiyo, umefika wakati wa kuwa kama wavuvi na si waomba samaki maana pamoja na kwamba mvuvi anakula samaki wote, ana uhakika kwamba atapata wengine kesho kwa kuwa anafahamu vyema kuvua kuliko anayesubiria kuomba.

Ikitokea siku mvuvi hajaenda kuvua, basi muomba samaki hatapata samaki. Lakini pia tukiwa kama mwomba samaki, tusile na kumaliza kama afanyavyo mvuvi maana hatuna uhakika wa kupata samaki kesho. Suluhisho pekee kwa mwomba samaki huyo ni kumwomba mvuvi amfundishe kuvua samaki na si kuendelea kuomba na kuishi kama ndege wa mwituni ambaye riziki yake inategemea safari zake za kila siku.

Maisha ya viongozi wetu yawe maisha ya watu wanaowaongoza. Raha, karaha, taabu na shida ziwe zetu sote kwa namna yoyote ile si kuwahimiza wananchi walipe kodi huku kukiwa na baadhi ya viongozi wakilalamikiwa kukwepa kodi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO



Na Adam Fungamwango

# Umeshawahi kukamata balanguru, balale?

NI ukweli usiopingika kuwa watoto wa zamani walikuwa watundu zaidi kuliko wa sasa. Walikuwa majasiri zaidi kuliko wa leo. Na walifanya vitu vingi kwa vitendo. Watoto wa sasa wamekuwa na akili nyingi, ambazo zimechangia na kukua kwa teknolojia. Pamoja na hayo, hawana ujasiri na wanafanya vitu vingi kinadharia zaidi kuliko vitendo.

Wengine wameniandikia na kunikumbusha kuhusu mchezo wa kukamata wadudu, kama panzi, balanguru na balale ambao ulikuwa maarufu sana kwa watoto wa zamani. Inawezekana mpaka leo bado wako wanaofanya hivyo, hasa vijijini, lakini kwa kiasi kikubwa mchezo huo umepungua sana. Zamani kuanzia mijini, mikoani mpaka vijijini, ulikuwa mchezo maarufu wa watoto wakati huo, hata miji mikubwa kama Dar es Salaam.

Jamaa mmoja akaniambia kuwa zamani wao walikuwa wakikusanyika watoto na kwenda porini, au sehemu yenye majani na nyasi nyingi kutafuta wadudu waitwao, panzi, balanguru na balale na wanawakamata kwa wingi. Lakini kwa sasa mtoto wake ambaye ana miaka kama ambayo yeye alikuwa anakwenda kuwakamata, anawaogopa.

Hiyo ikanisukuma kuandika makala hii leo. Wengi walioniandikia wakisema kuwahi kufanya mchezo huo, wakaonyesha kukumbuka mbali, sana na kutoa hadithi mbalimbali jinsi wao walivyokuwa wakifanya.

Mchezo wa kukamata wadudu hao ambao ni jamii ya nzige ulikuwa maarufu sana nchini Tanzania, hasa kwenye maeneo au mikoa ambayo wanalima mahindi na mazao mengine yanayofanana na hayo. Ulikuwa ukifanywa na watoto kuanzia miaka saba na kuendelea kutegemea mtoto mwenyewe makuzi yake, hadi kuja kuuacha mchezo huo.

Chini ya miaka hiyo walikuwapo, lakini mara nyingi walikuwa wakikatazwa, kwa sababu pia haikuwa rahisi sana kuwakamata wadudu hao. Ilihitaji utayari, ukakamavu, mbinu na uvumilivu wa hali ya juu. Na watoto walitembea kwa umbali mrefu. Wenyewe kwa wakati huo walikuwa wanaita 'kubaka balanguru'.

Wadudu hao walikuwa na majina mengi kulingana na maeneo au mikoa husika. Jamaa mmoja kutoka Ruvuma ameniambia wanaita 'limbala' au 'limbanguli'. Wenye babawa wekundu wanaitwa 'mambalanguli', wakati mwingine waliwaita 'mdede'. Kwenye mikoa ya Kaskazini, hasa Tanga wanawaitwa 'Nzie'. Kwingine wanaitwa Ng'aga na wakubwa zaidi wanaitwa 'Bungu'.

Hata hivyo wengi wao tuliwafahamu kama 'balanguru' au watoto wa Dar es Salaam wakatunga jina lingine 'balale'. Wote hao ni wadudu jamii ya nzige, wakiwamo panzi. Lakini watoto wa kipindi kile hawalipenda sana kuwakamata panzi kwa sababu walikuwa rahisi zaidi kuwapata kuliko balanguru.

Waliwahitaji zaidi hao kwa sababu kwanza ni wakubwa kuliko panzi, halafu haikuwa rahisi kuwakamata kwa sababu walikuwa wakijilinda na miiba mikali na wajanja sana kuruka na kuepuka hatari. Kukamata balanguru au balale ulikuwa ni ufahari mkubwa kwa mtoto wa miaka hiyo kuliko panzi. Kwa sababu unaonekana ni jasiri. Hakuna chochote walichokuwa wakipata watoto. Hawakuwa wakilipwa. Ilikuwa ni michezo tu ya kitoto. Ilikuwa ni kama burudani na walikuwa akijisikia raha sana na michezo ile.

Mwenye kukamata balale wengi ndiye mwamba, au mjanja kuliko wenzake. Watoto walitoka majumbani mwao na kutembea kwa umbali mrefu kwa kazi hiyo tu ya kusaka balanguru ambao walikuwa hata hawaliwi.

Hawakujali kutembea kwenye nyasi ndefu, kukatwa na majani yenye miba au kuchomwa na miiba, majani ya kuwasha hata kupambana na jua kali. Mvua na vikwazo vingi na hata wakati mwingine kukutana na wanyama wasumbufu pia hawakuogopa. Kuna wakati walikuwa wakinyimwa hata chakula nyumbani. Kwao wala haikuwa tatizo. Walichohitaji ni furaha ya moyo wao. Kuwakamata wadudu hao tu. Kwani ni furaha na faraja tosha kuliko chochote.

Jamaa mmoja alinimbia yeye na watoto wenzake wanane miaka ya katikati ya 1980, walitoka kwa miguu kutoka majumbani kwao Buguruni, hadi maeneo ya Jangwani kusaka balale na katika harakati hiyo alipoteza shati. Pamoja na kupata balale wengi, aliporudi nyumbani alitembezewa kichapo kwa kupoteza shati. Na kwa wakati huo ikumbukwe nguo zilikuwa adimu sana kuzipata.

Mwingine akaniambia kuna wakati wakitoka mapumziko shuleni wanafanya kazi ya kukamata balanguru na inafika wakati madaftari yanaanguka wao hawana bahari. "Kweli mkuu huu mchezo tulikuwa tunaupenda sana watoto wa miaka hiyo. Inafikia kipindi madaftari yanaanguka huna habari. Sasa ngoja urudi nyumbani. Upambane na kibano. Kwanza umechelewa kurudi shule, pili madaftari yamepungua," alisema mchangiaji huyo.

Yuko aliyekumbusha kuwa unakwenda kuwakamata balale kwenye nyasi ndefu sana na kuna mabua ya mahindi ambayo yamekauka, hivyo ukipita hovyo yanakata kama kisu. Yanaweka mikwaruzo kwenye ngozi, halafu jioni unakwenda kuoga. "Haki ya Mungu unawashwa utafikiri nini."

Mchangiaji mwingine yeye alikumbushua staili ya kubaka balanguru, akisema kuwa inabidi mkono uukunje kama kibakuli ili umkamate bila matatizo, kwa sababu wadudu hao ni waangalifu zao na wana miiba mikali ambayo mara nyingi ilikuwa ikiwachoma watoto. Aliyekuwa makini kuvumilia kuchomwa, mjanja, na kwenda umbali mrefu zaidi ndiye aliyewapata wengi zaidi.

"Mkuu watoto tunajipanga kwenye msitu wa majani kama tunakwenda vitani. Kumbe tupo bize kukamata balanguru. Lakini mtindo ule nadhani unasaidia watoto kuwa wakakamavu, wavumilivu, kujituma na kutokata tamaa kwenye maisha," alisema.


# HADITHI

# HADITHI

**KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa.**
**Donald, Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Anakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.**

# Sumu ya Mapenzi-22

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




"Vipi, hivi simu yako ilipona kweli?"

"Simu gani?"

"Kwani huna simu wewe?"

"Simu ina maana gani? Mimi si nimepona?"

"Kwa hiyo wewe huna simu hapo. Maana hata nikipiga haipatikani"

"Doroth, unapigaje simu wakati mimi nimelazwa hospitalini? Unanipigiaje simu?"

Kwani kuna nini?"

"He, baba basi, tufanye yameisha."

"Wewe badala ya kuangalia afya ya mgonjwa, unaulizia simu. Kwenye ajali simu inasalimika kweli? Kama haikuharibika, basi vibaka yatakuwa wameichukua." Doroth na dada yake waliondoka. Na wao walikuwa wa mwisho kumuona mgonjwa.

"Kwani simu ina nini?" Alianza kujiuliza Donald.

Alirudisha akili yake nyuma kabla ya ajali. Anachokumbuka ni kwamba simu yake ilikuwa imeisha chaji. Akakumbuka kuwa aliiweka kwenye droo ya gari. Mpaka sasa hakujua gari lake limeharibika kiasi gani.

Akakumbuka hajapoteza simu kwenye ajali hiyo, labda tu itakuwa imeharibika baada ya ajali. Ghafla alipata mgeni ambaye hakutarajia. Haukuwa muda wa kuangalia wagonjwa.

Ilishatimu saa 2:00 usiku. Kila mgonjwa alikuwa kitandani kwake. Alivaa nguo za kiraia kiasi cha Donald kumsahau. Alionekana kushangaa kupokea mgeni wa aina hiyo. Hata hivyo aliifananisha sura kama aliwahi kuiona mahali. Mgeni alitabasamu. Na yeye akatabasamu kwa kujilazimisha.

"Pole sana." Alikuwa mtu huyo aliyejipa mamlaka ya kuja kuangalia wagonjwa usiku.

Cha kushangaza ni kwamba hata wale walinzi ambao walikuwa wanamlinda, walimruhusu kiulaini.

"Nani huyu?" Alizidi kujiuliza.

"Unajisikiaje sasa?"

"Kidogo afadhali," alijibu.

"Naitwa Inspekta Andrew, nadhani unanikumbuka."

Hapo ndipo Donald alipokumbuka kuwa sura ile ilikuwa ya Inspekta Andrew na alimwona kwa mara ya kwanza na ya mwisho, siku alipokwenda kuhojiwa kuhusu kifo cha mpenzi wake Tausi.

Anakumbuka baada ya kuchukuliwa ofisini na Koplo Peter alipelekwa moja kwa moja hadi ofisini kwake. Na baadaye, ndiye aliyetoa idhini ya afande huyo kuanza kumhoji. Pia ndiye aliyetoa ruhusa ya kuachiwa na kuendelea na shughuli zake ingawa alitakiwa kufuata masharti kadhaa, ikiwamo kutosafiri nje ya Dar es Salaam.

**"Walitumwa kuchukua simu kwa sababu nilimsikia mmoja akisema, lazima simu ipatikane afikishiwe anayeitaka, vinginevyo kazi yote itakuwa ya bure. Na baada ya hapo sikusikia kitu tena. Fahamu zikapotea moja kwa moja."**

"Nimekuja kukujulia hali."

"Nashukuru mzee."

"Ila nataka tutete kidogo."

Hilo ndilo aliloona amekuja nalo na si kumjulia hali. Kama kujulia hali angekuja mapema. Alijia kabisa Inspekta Andrew amekwenda pale kikazi.

"Sawa, haina neno mzee."

Wakati huo wote Donald alikuwa amelala kitandani. Sehemu ya mguu wake wa kulia na mkono wa kushoto zilikuwa zimefungwa bandeji kutokana na majeraha aliyoyapata. Inspekta alikaa kwenye kitanda alicholalia Donald.

"Naomba kujua ajali uliyoipata kwa mtazamo wako unadhani ni ya kawaida, au ilikuwa kama ina mkono wa mtu?"

"Mkono wa mtu? Kwa nini afande unaona kama kuna mkono wa mtu?" Ilikuwa ni swali kwa swali.

"Mpenzi wako aliuawa. Mpaka sasa hatujajua watu hao walikuwa na nia gani? Na kwa sababu gani walifanya hivyo. Inawezekana mlengwa wa pili baada ya kifo cha Tausi ni wewe. We unaonaje?"

"Afande siwezi kusema ndiyo au hapana. Dunia ina mambo mengi."

"Mazingira ya ajali yalikuwaje?"

"Yaani ni vijana wanaocheza na pikipiki barabarani, ndiyo walionipoteza maboya. Walikuwa kama wanakuja usoni kwangu, nikawakwepa, ndiyo nikaenda pembeni, hadi kwenye korongo."

"Baada ya hapo?"

"Sikujua chochote kinachoendelea hadi nilipozinduka hapa hospitalini."

"Kwa hiyo hakuna chochote kisicho cha kawaida?"

"Nimekumbuka." Donald alijibu ghafla kama aliyekurupushwa kwenye usingizi.

"Kitu gani?"

"Kabla sijapoteza fahamu moja kwa moja pale kwenye ajali, kama kuna watu kwa mbali walifika pale na kuanza kubishana kuhusu simu."

"Simu?" Aliuliza Inspekta kwa mshangao.

"Ndiyo, niliwasikia kwa mbali wakinisachi, wakitafuta simu yangu."

"We unadhani ukipata ajali, vibaka wakiwahi hapo wanachotaka hasa ni nini. Lazima waanze na simu kwanza."

"Sawa Inspekta, najua hilo lakini ilionekana kabisa walivamia hapo kwa lengo la kutaka simu tu na kwa jinsi walivyoongea ilionekana kabisa huenda kuna kitu."

"Kitu gani?"

"Walitumwa kuchukua simu kwa sababu nilimsikia mmoja akisema, lazima simu ipatikane afikishiwe anayeitaka, vinginevyo kazi yote itakuwa ya bure. Na baada ya hapo sikusikia kitu tena. Fahamu zikapotea moja kwa moja."

"Ina maana wakaichukua."

"Sijajua kwa sababu nilizirahi, lakini haikuwa mfukoni. Ilikuwa kwenye droo ya gari. Na gari sijui liko kwenye hali gani."

"Gari liko Makao Makuu ya Polisi lakini imeharibika sana."

"Basi Inspekta naomba mkaangalie kwenye droo, kama mtaikuta simu, basi ilete hapa kuna kitu nataka kukuelekeza cha kufanya. Lakini hata kama hukuipata, njoo tukae tujue nini tutafanya."

"Okay, nitatuma vijana wangu, waifanye kazi hiyo. Vipi inaonekana kuna siri yoyote kwenye simu yako?"

"Sijajua, lakini naona ni kama hao watu kuna kitu wanatafuta ndani ya simu yangu ambacho mimi sikijui." Donald aliongopa.

Donald alianza kuwa na hofu na Doroth. Alionekana kuuliza zaidi habari ya simu. Lakini akakumbuka kuwa kuna watu walivamia kwenye ajali hiyo na kuitaka simu hiyo hiyo.

Hii ndiyo sababu iliyomfanya amwambie inspekta Andrew kwa sababu alianza kuhofia usalama wake. Aliona huenda ajali ile ilitengenezwa kwa lengo la kumuua, au kuipata simu ambayo mtu aliye nyuma ya hilo ana wasiwasi kuwa imeficha siri fulani.

"Sasa kwa nini asikodi watu tu wakanivamia na kuninyang'anya, hadi asababishe ajali ya kutengeneza?" alijiuliza.

Hapo ndipo wazo lingine likaja kuwa huenda anatakiwa auawe ili siri ifichike.

Kichwa kilizidi kumuuma kwa kuwaza vitu vingi kwa wakati mmoja. Na hii ilimfanya aingiwe na hofu, hivyo kutaka jambo hili liishe mapema zaidi. Kuliacha kama lilivyo lingeweza kusababisha apoteze maisha bila polisi kufahamu nini kilisababisha mpenzi wake Tausi auawe.

**INAENDELEA JUMAPILI**

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI

HOME

AWAY

BRAZIL

2.00 | 3.14 | 3.62

ARGENTINA

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# DRAKE, SOULJA BOY HOFU TUPU WAKIZINDUA ALBAM ZAO MPYA

PENGINE bifu la aina yake linaweza kuibuka kati ya marapa wawili maarufu wa Marekani, Drake na Soulja Boy, ambao hivi karibuni walizindua albam zao mpya kwa wakati mmoja.


Tukio hilo ambalo si la kawaida kufanywa na wanamuziki wakubwa, limeonekana kama mwendelezo wa ugomvi na hatimaye kuibua makundi hasimu.

Hata hivyo, Drake ameonekana kukata kiu ya mashabiki wake baada ya kuachia rasmi album yake Certified Lover boy (CLB) ambayo ina jumla ya nyimbo 21.

Ndani ya Albam hiyo amewashirikisha wasanii wengine kama Jay Z, Lil Wayne, Future, Young Thug, Lil baby, Lil Durk, Travis Scott na Tems.

Kwa upande wa Soulja Boy, ameachia albam yake mpya inayoitwa SWAG4, ambayo ina jumla ya vibao 14.





# *Mitindo jezi mpya Simba gumzo*

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamissa Mobetto, ametumika vilivyo kunogesha kwa kuonyesha mitindo mipya ya jezi ya Simba, ambazo zitavaliwa na mashabiki wa kike.

Hamissa, alitupia jezi za aina tatu za timu hizo ambazo ni maalum kwa wanawake ikiwamo ile fupi maarufu kama 'kitopu' ambayo ilimpa muonekano wa kuvutia.

Katika ubunifu uliofanywa na Simba ni kutengeneza jezi hizo ambazo huvaliwa na mashabiki wa kike hasa katika kipindi cha joto.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




# RIQUELME ASEMA MESSI ATASHINDA UEFA NA PSG




**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi atashinda Ligi ya mabingwa Ulaya na Paris Saint-Germain kabla ya kustaafia soka Barcelona, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani, Juan Roman Riquelme.

Messi alijiunga na miamba hao wa Ligue 1 kwa mkataba wa miaka miwili mwezi uliopita baada ya kumaliza muda wake kule Barca, akiichezea kwa mara ya kwanza timu hiyo akitokea benchi kwenye ushindi wa 2-0 dhidi ya Reims.

Huku PSG ikiwa imetawala soka la Ufaransa kwa kipindi cha muongo mmoja ikishinda mataji saba ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, pamoja na Coupe de France na Coupe de la Ligue mara sita kwa kipindi hicho - taji la Ligi ya mabingwa Ulaya, limekuwa gumu kwao.

Riquelme ambaye alicheza pamoja na Messi katika klabu na timu ya taifa ya Argentina, anaamini mchezaji mwenzake huyo atatwaa kombe la Ligi ya mabingwa Ulaya akiwa na PSG.

Lakini wakati huo huo, kiungo huyo wa zamani hafikirii kama Messi amemaliza muda wake kule Barcelona.



# *Edu awataka mashabiki Arsenal kuvumilia*

**LONDON,** England

EDU amewashauri mashabiki wa Arsenal kuwa na uvumilivu huku akiangalia namna ya kuendelea kufanya kazi na Mikel Arteta kujenga mtazamo mpya wa timu hiyo iliyojaa vijana.

Arsenal walitumia fedha nyingi kwenye usajili uliopita, wakiwachukua Nuno Tavares, Albert Sambi Lokonga, Ben White, Martin Odegaard, Aaron Ramsdale na Takehiro Tomiyasu.

Waliokuwa wanalipwa mshahara mkubwa, David Luiz na Willian wote wameondoka, huku Joe Willock akiuzwa kule Newcastle United na Hector Bellerin akipelekwa kwa mkopo Real Betis.

Arsenal waliikatalia Everton mpango wao wa kutaka kumsajili, Ainsley Maitland-Niles, licha ya mchezaji huyo kuonesha nia ya kutaka kuondoka hadharani, lakini Reiss Nelson, Matteo Guendouzi, Lucas Torreira, Runar Alex Runarsson na William Saliba wote wakiwa wameondoka kwa mkopo.

Hata hivyo, vipigo vitatu katika mechi za ufunguzi wa Ligi Kuu England, kumewafanya Arsenal kuwa chini kwenye msimamo wa Ligi, huku wakiwa hawajafunga bao hata moja.

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 05 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4502 | Maastricht vs Telstar | 2.50 | 3.43 | 2.55 |
| 16:00 | 2557 | Levanger vs Arendal | 2.23 | 3.59 | 2.72 |
| 16:00 | 3565 | Rwanda vs Kenya | 2.32 | 2.95 | 3.45 |
| 16:00 | 4089 | Norrby IF vs Vasalunds IF | 1.65 | 4.09 | 4.79 |
| 16:00 | 4120 | PK-35 vs Jippo | 1.72 | 3.44 | 4.46 |
| 16:00 | 4185 | Belarus vs Wales | 6.20 | 3.70 | 1.59 |
| 16:00 | 4552 | Sweden vs Uzbekistan | 1.32 | 5.20 | 9.01 |
| 17:00 | 1478 | Burgos vs Valladolid | 3.55 | 2.86 | 2.25 |
| 17:00 | 2030 | Independiente Fbc vs CA 3 De Febrero | 2.17 | 3.25 | 3.45 |
| 17:00 | 2110 | Moss vs Floya | 1.48 | 4.56 | 5.05 |
| 17:00 | 2229 | Nueva Chicago vs Belgrano Cordoba | 3.83 | 2.81 | 2.09 |
| 17:00 | 2873 | Mitre SdE vs Estudiantes Rio Cuarto | 2.91 | 2.76 | 2.57 |
| 17:00 | 4004 | Resistencia FC vs Sportivo Ameliano | 1.96 | 3.10 | 3.83 |
| 17:00 | 4415 | Flekkeroy vs Notodden | 1.95 | 3.54 | 3.34 |
| 17:00 | 5398 | Dalkurd FF vs Sandvikens IF | 2.40 | 3.65 | 2.70 |
| 17:00 | 5881 | UD Ibiza Eivissa vs Amorebieta | 2.07 | 3.00 | 3.88 |
| 17:30 | 1407 | Lida vs Belshina | 5.98 | 4.15 | 1.46 |
| 17:45 | 4048 | ADO Den Haag vs FC Eindhoven | 1.98 | 3.70 | 3.50 |
| 18:00 | 1817 | Assyriska vs Gefle IF | 3.74 | 3.74 | 1.79 |
| 18:00 | 2263 | CA Atlanta vs Gimnasia Mendoza | 2.76 | 2.76 | 2.71 |
| 18:00 | 5373 | KamAZ vs Tom Tomsk | 2.26 | 2.90 | 3.24 |
| 18:00 | 5753 | Puerto Montt vs CD Santa Cruz | 2.10 | 3.40 | 3.50 |
| 18:30 | 1602 | IFK Mariehamn vs KuPS Kuopio | 5.63 | 4.17 | 1.48 |
| 18:30 | 1706 | Foggia vs Potenza SC | 2.41 | 3.18 | 2.93 |
| 18:30 | 2457 | CD Ebro vs Badalona | 2.11 | 3.20 | 3.25 |
| 18:30 | 4369 | Lucchese vs Cesena | 3.02 | 2.92 | 2.52 |
| 18:30 | 5039 | Gubbio vs Fermana FC | 2.13 | 3.12 | 3.57 |
| 19:00 | 1733 | England vs Andorra | 1.04 | 13.15 | 41.54 |
| 19:00 | 2574 | Once Caldas vs Atletico Bucaramanga | 2.37 | 3.15 | 2.81 |
| 19:00 | 2878 | Iceland vs North Macedonia | 2.19 | 3.34 | 3.29 |
| 19:00 | 3951 | Togo vs Namibia | 2.60 | 2.90 | 3.05 |
| 19:00 | 4031 | Albania vs Hungary | 3.16 | 2.91 | 2.51 |
| 19:00 | 5836 | Bulgaria vs Lithuania | 1.52 | 3.96 | 6.62 |
| 19:15 | 1032 | Alcorcon vs Zaragoza | 2.40 | 2.77 | 3.36 |
| 19:15 | 1247 | Mirandes vs Las Palmas UD | 2.56 | 2.85 | 3.00 |
| 19:30 | 4139 | Godoy Cruz vs Gimnasia y Esgrima | 2.19 | 3.20 | 3.06 |
| 19:30 | 5415 | Patronato Parana vs Talleres | 3.06 | 3.01 | 2.30 |
| 20:00 | 1872 | CF Atlante vs Leones Negros Udg | 1.71 | 3.44 | 4.56 |
| 21:00 | 4382 | Dordrecht vs VVV Venlo | 2.98 | 3.52 | 2.15 |
| 21:00 | 5268 | Deportivo Pasto vs Deportivo Cali | 3.10 | 2.86 | 2.36 |
| 21:45 | 1955 | Spain vs Georgia | 1.09 | 9.22 | 28.05 |
| 21:45 | 2295 | San Marino vs Poland | 45.03 | 22.01 | 1.01 |
| 21:45 | 2777 | Switzerland vs Italy | 3.82 | 3.43 | 1.97 |
| 21:45 | 3490 | Belgium vs Czech Republic | 1.44 | 4.50 | 7.00 |
| 21:45 | 4215 | Kosovo vs Greece | 3.61 | 3.11 | 2.17 |
| 21:45 | 4548 | Germany vs Armenia | 1.09 | 9.59 | 23.96 |
| 21:45 | 4648 | Romania vs Liechtenstein | 1.05 | 13.09 | 35.23 |
| 22:00 | 4309 | Brazil vs Argentina | 2.00 | 3.14 | 3.62 |
| 22:00 | 5517 | Gabon vs Egypt | 2.97 | 2.82 | 2.48 |
| 23:00 | 4193 | Independiente Medellin vs Independiente Santa Fe | 2.32 | 2.94 | 3.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# CAMAVINGA: NDOTO YANGU IMETIMIA KUTUA MADRID

## ●●● Aliweka rekodi ya mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea timu ya...

**MADRID,** Hispania

EDUARDO Camavinga amesema kwamba, uhamisho wake wa kwenda Real Madrid ni ndoto iliyotimia baada ya kujiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kutoka Rennes siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto.

**Camavinga alisaini mkataba wa miaka sita na Madrid kwa dili lililoripotiwa kuwa na thamani ya euro milioni 45, awali akiwa anahusishwa na Manchester United na Paris Saint-Germain.**

Baada ya uhamisho huo mkubwa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 raia wa Ufaransa ameelezea furaha yake ya kutua hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

"Ni ndoto niliyokuwa nayo wakati nikiwa mtoto. Siwezi kusubiri kuona namna nitakavyoingia uwanjani, kitu ambacho ni hamasa kubwa kwangu," alisema Camavinga.

"Natumaini kucheza hapa haraka inavyowezekana, kwani kazi imeshakamilika."

Camavinga alicheza mechi 71 za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiwa na Rennes na jumla ya 88 kwenye mashindano yote tangu alipoanza kuichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2019.

Katika umri wake wa miaka 18 na miezi tisa, yeye ni mchezaji mwenye umri mdogo zaidi aliyecheza mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, tangu Basile Boli ambaye aliweka rekodi hiyo mwaka 1985.

Akiichezea timu ya taifa ya Ufaransa kwa mara ya kwanza Septemba 8, mwaka jana, Camavinga aliweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea timu hiyo tangu Maurice Gastiger alipofanya hivyo dhidi ya Luxembourg miaka 107 iliyopita.

Ni Gastiger pekee (akiwa na miaka 17 na miezi mitano) aliifungia Les Bleus katika umri mdogo zaidi kuliko Camavinga, ambaye alikuwa na umri wa miaka 17 na miezi 11 akifunga dhidi ya Uswisi Oktoba mwaka jana.

"Uhamisho wangu wa kutua Real Madrid umefanyika kwa haraka zaidi. Nina furaha kubwa na najisikia fahari kwa hilo," alisema Camavinga.

## ZISIKUPITE

### TRAORE MSHAHARA JUU

KLABU ya Wolves inataka kumfanya winga wa Hispania, Adama Traore, 25, kuwa mchezaji wao anayelipwa mshahara wa juu zaidi kwa malipo ya pauni 120,000 kwa wiki kuzuia nia za klabu za Tottenham na Liverpool kumchukua. ***(Sun)***

### MADRID NA MBAPPE

REAL Madrid waliandaa mikataba saba ya kufanya mazungumzo na Kylian Mbappe,22, huku wakiazimia kusaini mkataba na mshambuliaji huyo Mfaransa kabla ya muda wa mwisho wa kipindi cha uhamisho kutimia, lakini timu hiyo ya Hispania ina matumaini makubwa kuwa atajiunga nao kutoka Paris St-Germain mwaka 2022. ***(Sport)***

### AIKOSESHA FEDHA KLABU

KUSHINDWA kwa Kylian Mbappe kuhama kutoka PSG msimu huu kuliifanya klabu yake ndogo ya AS Bondy kukosa gharama ya fidia zaidi ya euro milioni 2. ***(L'Equipe)***

### CAMAVINGA ALIPEWA OFA NZURI

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Eduardo Camavinga, 18, aliishawishi Rennes kumuacha ajiunge na Real Madrid msimu huu licha ya kwamba PSG ilitoa ofa nzuri zaidi kwake binafsi. ***(AS)***

### PSG HAIKUMTAKA RONALDO

KLABU ya PSG haikuwasilisha dau kwa ajili ya mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 36, licha ya kufanya mazungumzo juu ya uhamisho wa mchezaji huyo kabla ya kujiunga na Manchester United. ***(Le10Sport - in French)***

### DYBALA NA JUVENTUS

JUVENTUS sasa wamejiimarisha zaidi kumtumia Paulo Dybala, 27, kama mchezaji wao muhimu zaidi, baada ya kukubali kumuacha Cristiano Ronaldo arejee Manchester United. ***(Calciomercato)***

### LINGARD ALIIKATALIA WEST HAM

KIUNGO wa kati wa England, Jesse Lingard, 28, alikataa fursa ya kujiunga na West Ham kwa mkataba wa kudumu baada ya muda wake wa mkopo kumalizika msimu uliopita, ili kupigania nafasi yake Manchester United. ***(90Min)***

### LENO AWANIWA INTER

KLABU ya Inter Milan ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mlindalango wa Arsenal na Ujerumani, Bernd Leno, 37, ambaye anatarajiwa kuondoka kwa washikabunduki hao kwa uhamisho huru wakati mkataba wake utakapomalizika msimu ujao. ***(Tuttosport - in Italian)***

### OLMO ATAKIWA BARCELONA

BARCELONA itajaribu kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo, 23, kutoka klabu ya Ujerumani ya RB Leipzig, Januari, ambapo wamekubali kumpatia mkataba wa miaka mitano. ***(Mundo Deportivo)***

### BAKAYOKO KUBAKI

KIUNGO wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko, 27, ana matumaini ya kuendelea kubaki katika klabu ya AC Milan baada ya mkataba wake wa mkopo kutoka Chelsea kumalizika. ***(Goal)***

## Ligi ya netiboli taifa kupigwa Morogoro

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO mpira wa netiboli Ligi daraja la pili ngazi ya Taifa yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Septemba 19 hadi 29, mwaka huu mkoani Morogoro, ambayo yatashirikisha klabu tatu kutoka kila mkoa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Chama cha mchezo huo (CHANETA), Devota Minja, alisema maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na kila timu inafanya mazoezi ili kujiweka sawa kuelekea katika mashindano hayo.

"Timu zote zinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kuelekea katika mashindano hayo, tunaomba kila kiongozi asisitize wachezaji wake kufanya mazoezi mpaka hapo tutakapowatangazia siku rasmi ya kuripoti sehemu husika ya mashindano,"alisema Devota.

Alisema kuwa kwa timu ambazo zitafanya vizuri katika mashindano hayo zitapandishwa daraja na kushiriki Ligi daraja la Kwanza ambapo aliweka wazi kuwa wanahitaji jumla ya timu 8, wakiwa na lengo la kuuendeleza zaidi mchezo huo.

Mbali na mashindano hayo alisema watakuwa na mashindano ya Kombe la Nyerere yatakayofanyika Oktoba 14, mwaka huu, ambayo yataambatana na uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 16, mwaka huu mkoani Dodoma.

## Serikali kuwekeza kwenye michezo

**Na Saada Akida**

SERIKALI imepanga kufanya mageuzi makubwa katika medani ya michezo na burudani kwa uwekezaji mkubwa .

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema kutokana na kilio kutoka kwa wadau wa michezo, serikali imepanga kuanza kwa kurekebisha miundombinu na ufadhili ili kuifanya michezo kukua zaidi.

Alisema katika mageuzi hayo ni kusukuma mambo ya kimkakati katika sekta ya michezo isonge mbele kwa kuwekeza katika fedha, kwa kuchukuwa asilimia 5 katika michezo ya kubashiri.

"Tayari hizo fedha zimeshatengwa na tumeshapeleka barua Wizara ya Fedha ndani ya mwezi huu (Septemba) fedha hizo ziweze kuwekwa katika akaunti ya maendeleo ya fedha za michezo," alisema Abbas.

Alisema katika kuhakikisha wanafikia mageuzi hayo serikali ina haja ya kutafuta vyanzo vya fedha ili kuendeleza michezo hiyo kwa kuhakikisha timu za taifa zinapata mahitaji muhimu ikiwamo fedha za safari na malazi pamoja kuangalia zaidi miundombinu.

"Hivi karibuni tutaunda kamati ya kusimamia fedha za michezo ili kufikia malengo yetu, ikiwamo timu zetu za taifa ziwe zinafikiria ushindi tu na sio masuala ya posho au jinsi ya kufika katika mashindano husika,"alisema.

# JKU YAANZA KUWARUDISHA WACHEZAJI WALIOWATOA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU S.C imesema katika msimu mpya wa ligi wanatarajia kuwarejesha wachezaji wake waliowatoa msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa JKU, Omar Khamis Matu amesema wapo wachezaji wao ambao msimu uliopita waliwapeleka katika klabu mbalimbali, hivyo wanatarajia kuwarejesha ili kuitumikia timu yao hiyo kwa msimu huu.

**Kocha huyo hakutaka kuyaweka wazi majina wala idadi ya vijana wanaokusudia kuwarejesha klabuni hapo mara baada ya dirisha la usajili kuwekwa wazi.**

Alisema msimu huu utakuwa wenye ushindani kwakuwa tayari ligi ya Zanzibar imeshapata mdhamini, hivyo lazima wawe makini katika kusajili wachezaji.

"Tunatakiwa tuwe makini katika kufanya usajili wa wachezaji wenye viwango, na kwa hatua ya awali tutaanza kuwarejesha baadhi ya wachezaji wetu, lakini pia tutafanya usajili kuongeza nguvu kikosi chetu kuelekea msimu mpya wa ligi," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa timu hiyo inaendelea na mpangilio wake wa mazoezi mepesi katika kuelekea msimu wa ligi ambapo wanasubiri Shirikisho la soka la Zanzibar, ZFF, litangaze kalenda ya mashindano kwa msimu huu.

Ligi Kuu ya Zanzibar msimu wa 2021 /2022 imedhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya vijana, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Mwakinyo atoa siri kumpiga Mnamibia*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa hapa nchini, Hassan Mwakinyo ambaye amefanikiwa kuutetea mkanda wake wa Ubingwa wa Afrika (ABU ) uzito wa Super Welter, ametoa siri ya kumpiga mpinzani wake Julius Indongo TKO.

Mwakinyo (pichani) aliibuka mshindi dhidi ya bondia huyo raia wa Namibia katika pambano la raundi 12 lililofanyika juzi.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa pambano hilo, Mwakinyo alisema siri kubwa ya kuibuka na ushindi huo ni ushirikiano aliopewa na familia yake pamoja na mbinu za Kocha wake mkuu.

"Ninashukuru nimeweza kupata ushindi kwa kumpiga mapema mpinzani wangu, sio kazi rahisi kumpiga bondia mzuri kama huyu, kwani ana uwezo mkubwa kutokana na mapambano makubwa ambayo aliyacheza na kufanya vizuri," alisema Mwakinyo.

Hata hivyo, bondia huyo aliongeza kuwa anawashukuru Watanzania na mashabiki wake ambao walijitokeza kwa wingi kumpa sapoti.

Mwakinyo alisema lengo ni kuendeleza kiwango chake na kufikia hadhi ya juu kama walivyo mabondia wengine ambao wanacheza ngumi za kulipwa nje ya nchi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, alisema amefurahishwa na ushindi huo na kudai mara baada ya kufika mkoani humo atampa zawadi ya fedha ambazo hakuweza kuzitaja kuwa ni kiasi gani.

"Kabla ya pambano Mwakinyo aliniahidi kufanya vizuri na kweli amefanya kama alivyoniambia, hivyo nitampa zawadi ya fedha ambayo hapa siwezi kutaja ni kiasi gani mpaka hapo nitakapomkabidhi tutakapofika Tanga," alisema Malima.

# Michezo

Jumapili Septemba 5, 2021

Nipashe




Camavinga: Ndoto imetimia kutua Madrid UKURASA 22



Nahodha wa Argentina, Lionel Messi, akiwania mpira dhidi ya golikipa wa Venezuela, wakati wa mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 baina ya timu hizo, katika uwanja wa Olímpico mjini Caracas, juzi. Argentina ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDANO**

# Simba hiyo Karatu

Yaenda kuweka kambi huko na itacheza mechi mbili za kirafiki, itarudi siku tatu kabla ya tamasha na...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinaondoka leo kuelekea Karatu mkoani Arusha kwa ajili ya kambi ya awamu ya pili kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika 2021/22.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ezikiel Kamwaga, alisema timu inaondoka leo ikiwa na wachezaji 23 na wale waliokuwa katika majukumu ya taifa wataungana baada ya kurejea.**

Alisema timu hiyo itakuwapo Karatu kwa kambi ya awamu ya pili na kurejea siku tatu kabla ya kucheza mechi yao ya kirafiki ya kimataifa kwenye kilele cha tamasha lao la Simba Day.

"Wachezaji wamekutana leo (jana) na kesho (leo) wanasafiri kuelekea Karatu, Arusha kwa ajili ya awamu ya pili ya kambi yetu na kurejea siku tatu kabla ya tamasha letu," alisema Kamwaga.

Alisema kuhusu mechi ya kirafiki bado hajapewa taarifa kutoka benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Didier Gomes, ambao watacheza wakiwa kambini huko.

Kamwaga (pichani) alisema baada ya timu kurudi kutoka Morocco wachezaji walipewa mapumziko ya siku chache na wamerejea na wanaondoka moja kwa moja kuelekea Karatu, Arusha, katika maandalizi ya awali ya pili ya kambi yetu.



Alisema maandalizi ya tamasha lao yanakwenda vizuri na Septemba 13, mwaka huu, wiki ya Simba itaanza kwa kufanya shughuli za kijamii kwa ajili ya kuanza siku ya Simba Day ambalo inafanyika kila mwaka.

Taarifa zilizoifikia gazeti hili ni kwamba kwa siku 13 ambazo Simba watakuwa kambini watacheza mechi zisizopungua mbili huku ikitajwa kucheza dhidi ya Namungo FC ambao nao wameweka kambi Karatu, pamoja na timu mmoja kutoka nchini Kenya.

Simba ilikuwa kambini Morocco, ikicheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya FAR Rabat na Olympique Club de Khouribga ambayo yote iliisha kwa sare.

## Simba Queens: Tunataka ubingwa

**Na Somoe Ng'itu,** NAIROBI

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa CECAFA, wawakilishi wa Tanzania waliobakia katika michuano hiyo, Simba Queens kutoka jijini Dar es Salaam, wamesema malengo yao ni kuchukua ubingwa.

Bingwa wa michuano hiyo ndio atapata tiketi ya kuiwakilisha CECAFA katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zitakazochezwa Novemba mwaka huu nchini Misri.

Simba Queens itakutana na wenyeji Vihiga Queens katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza ya michuano hiyo hapo kesho wakati nusu fainali ya pili itawakutanisha Commercial Bank of Ethiopia dhidi ya Lady Doves FC kutoka Uganda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kufanya vizuri kwenye hatua ya makundi na anaamini wataendelea na ari hiyo katika mchezo unaofuata wa nusu fainali.

Hababuu alisema wamejiandaa kupambana kwa ajili ya kuhakikisha wanashinda na kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika.

Kocha huyo alisema wanajua wapinzani wao pia wamejiandaa kusaka ushindi, hivyo mchezo huo hautakuwa mwepesi kwa kila upande.

"Tutapambana kama ambavyo tumefanya katika mechi zilizopita, sasa tunaingia kwenye hatua ya mtoano, tunahitaji ushindi tu ili tufike fainali, " alisema Hababuu.

Aliongeza kuwa wamejiandaa kucheza kwa tahadhari kwa sababu wanakutana na wenyeji ambao wana faida ya kutumia uwanja wa nyumbani.

Mshambuliaji wa Simba Queens, Oppa Clement aliliambia gazeti hili ndoto ya wachezaji wote wa timu hiyo ni kubeba ubingwa na kuweka rekodi ya kushinda taji la michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

"Tunataka kwenda katika fainali huko Misri, ndio sababu kubwa ya kupambana ili tuwe mabingwa, hatuhitaji kuikosa nafasi hiyo muhimu," alisema mshambuliaji huyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >